Leo yetu ndiyo kesho yetu
# Uelekeo




MICHEZO
## Yanga yawashukuru mashabiki waliojitokeza Lubumbashi
Uk.24




AFYA
UK.11

AFYA
## DALILI ZA UGONJWA WA GOUT, TIBA NA NAMNA YA KUJIKINGA
Uk. 10




Toleo Na. 00008 | Jumatano Aprili 5 - 11, 2023 |

# Wanafunzi wapigwa `stop' masomo wakituhumiwa kwa ushoga, usagaji



## ...Waislamu Singida wajipanga kuandamana
Uk. 4

HABARI UK.4



# Simba, Yanga sasa zatinga makanisani
Uk. 3

HABARINDANI



## Kabudi ataka waathirika wa ubakaji wafidiwe
Uk. 5

# MVTCC kuzalisha walimu wa Veta 660 kila mwaka

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro (MVTCC), 'kinatembea' na kasi ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika kuzalisha walimu wa ufundi stadi kikijipanga kuzalisha kada ya wataalam hao, 660 kila mwaka.

Akizungumza na Uelekeo kwa njia ya simu jana, Mkuu wa chuo hicho, Samwel Kaali, alisema wameandaa mpango mkakati wa miaka mitano kuanzia mwaka 2023/24 hadi 2027/28, kuhakikisha kwamba ujenzi wa vyuo vya ufundi kila wilaya, haukwami kwa sababu ya walimu wa ufundi.

Alisema wameandaa mpango mkakati utakaowezesha kutoa walimu 3,100 ndani ya miaka mitano ili kukidhi mahitaji ya nchi.

Alisema ili kufanikisha hilo, wameongeza udahili kutoka wanafunzi 120 kwa mwaka hadi 660 na kwamba utekelezaji wake utaanza mwaka huu wa fedha.

Alisema wameandaa kozi ya stashahada ya uzamili ya elimu ya ualimu wa ufundi na ufundi stadi (post graduate diploma in technical and vocational teacher education), inayotolewa kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Huria.

Kaali alisema kuanzia mwaka huu wa fedha, MVTCC inaanzisha stashahada ya walimu wa ufundi na ufundi stadi (diploma in engineering with technical and vocational teacher education).

"Programu tunazoendelea nazo ni cheti cha walimu wasaidizi wa ufundi stadi, stashahada ya walimu wa ufundi na ufundi stadi ambazo ni maalum kwa mafundi ambao wanataka kuwa walimu wa ufundi," alisema.

Kaali alisema tayari chuo kimeandaa mazingira ya kupokea idadi hiyo ya wanafunzi na tayari wameongeza hosteli na vyumba vya madarasa.

"Tunaongeza karakana mbili za ufundi wa uchakataji wa chakula na kozi ya urembeshaji na utiaji nakshi. Tunaenda kukarabati na kuweka vifaa vipya kwenye karakana nne zilizopo, tunatanua maktaba na kujenga kituo cha teknolojia za kidigitali," alisema Kaali. Alisema mpango wa muda mrefu wa mamlaka ni kujenga chuo kingine cha ualimu wa ufundi stadi kwa kuwa eneo la MVTCC ni dogo.

Mpango huo wa MVTCC unakuja wakati ambao serikali imeanza kujenga vyuo vya ufundi stadi kila wilaya nchini. Katika mwaka huu wa fedha, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongoza na Dk. Samia, ilitenga Sh. bilioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi huo.




**Moja ya majengo na eneo la kuegesha magari katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.**

# Maegesho ya magari KIA kupanuliwa kwa bil. 2.7/-

**Na Claud Gwandu, Arusha**

TATIZO sugu la maegesho ya magari katika Uwanja wa Ndege wa Kilimanjarto (KIA), huenda likawa historia baada ya mamlaka inayosimamia uwanja huo kuanza mradi wa upanuzi wa maegesho hayo utakaogharimu mabilioni ya Shilingi.

Mradi huo utakaotumia zaidi ya Sh. bilioni 2.7, utasaidia kuongeza uwezo wa maegesho ya magari katika uwanja huo unaochukua magari 85 kwa wakati mmoja kwa sasa na kufikia magari 180 kwa wakati mmoja katika uwanja huo wa pili kwa ukubwa nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo la Uwanja huo (KADCO), Christine Mwakatobe, alisema hivi karibuni kuwa maegesho hayo mapya yatasaidia kupunguza msongamano na tatizo sugu la ukosefu wa maegesho linalowakabili wenye magari wanaosafirisha abiria kwenda na kurudi katika uwanja huo.

"Ni tatizo sugu na kwa sasa maegesho yetu yana uwezo wa magari 85 tu wakati magari yanaongezeka karibu kila siku kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii, hivyo mradi huu utakapokamilika utakuwa ahueni kubwa kwa wageni wetu," alisema na kuongeza:

"Kwa nafasi hii finyu iliyopo, changamoto ya maegesho ilikuwa kubwa mno hapa,kwani kuna wakati tulikuwa tunapokea zaidi ya magari 300 kwa wakati mmoja kutokana na wingi wa wageni. Sasa fikiri changamoto ilivyokuwa kubwa na kuwa kero si kwa madereva tu, bali hata wageni ambao wanapenda kutumia uwanja wetu," alisema Christine na kuongeza:

"Mradi huu utasaidia madereva kupunguza muda mwingi wa kuwa ndani ya vyombo vyao vya usafiri kutafuta maegesho ambako wanachoka kabla hata ya kupakia wageni, hivyo utatoa fursa kwa madereva hao kuwahudumia vizuri wageni.

Alisema tayari mkandarasi wa kuongeza maegesho hayo ameshaanza kazi baada ya taratibu zote za kisheria kukamilika, na kwamba uwanja utakuwa na uwezo wa kuhudumia magari ya wageni, wafanyakazi wa uwanja na yale yanayosafirisha mizigo hasa ya mbogamboga na matunda kwenda masoko ya Ulaya yanayotumia uwanja huo.

> **Mradi huu utasaidia madereva kupunguza muda mwingi wa kuwa ndani ya vyombo vyao vya usafiri kutafuta maegesho ambako wanachoka kabla hata ya kupakia wageni...**

Mazao ya mbogamboga, matunda na maua, huzalishwa kwa wingi katika ukanda wa miteremko la Mlima Meru mkoani Arusha na pia mkoani Kilimanjaro na husafirishwa kwa wingi kupitia uwanja huo na kupelekwa katika masoko yaliyoko katika nchi za Umoja wa Ulaya.

Kwa nyaraka za mujibu wa mradi huo, pamoja na kuimarishwa kwa mitaro ya maji uwanjani hapo, mradi huo pia utaongeza idadi ya taa zitakazotumika uwanjani hapo, kuweka lami na kukarabati na kupanua sehemu ya maegesho ya magari uwanjani hapo.

Mradi huo, kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji huyo, utatoa ajira ya muda kwa vijana 100 kutoka maeneo yanayouzunguka uwanja ambao ulijengwa makusudi kwa ajili ya kuhudumia watalii wanaomiminika Kanda ya Kaskazini kushuhudia vivutio mbalimbali katika Hifadhi za Serengeti, Mlima Kimanjaro, Tarangire, Manyara na Arusha pamoja na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).




# Simba, Yanga sasa zatinga makanisani

BAADHI ya makanisa jijini Dar es Salaam, yameanzisha mfumo mpya wa ukusanyaji sadaka kutoka kwa waumini kwa kuwashindanisha kutokana na ushabiki wa mpira wa miguu kwa timu mbili maarufu nchini, Simba na Yanga.

Mfumo huo mpya wa ukusanyaji sadaka, unawafanya washabiki wa pande hizo mbili mahasimu, kutoa sadaka kwa kushindana na hatimaye kubaini ni upande gani utaibuka kidedea kwa kutoa sadaka kubwa zaidi.

Hali hiyo ilishuhudiwa katika Kanisa moja Katoliki Parokia (jina limehifadhiwa) iliyoko katika Wilaya ya Ubungo jijini Dar es Salaam Jumapili iliyopita.

Katika ibada zake tatu zilizofanyika siku hiyo, kila ibada ilitumia mfumo huo na kufanikiwa kukusanya sadaka kiasi cha kutosha kwa waumini wa Simba na Yanga ambapo upande wa washabiki wa Yanga, uliibuka mshindi kwa kutoa kiasi kikubwa cha sadaka. Aidha, Paroko na Msaidizi wake, wao walitangaza kanisani kuwa hawana timu (neutral), na hivyo nao liliwekwa kapu lao maalum ambapo kwa washabiki wasio na timu, walitumbukiza humo.

Hata hivyo, katika ibada zote tatu, kapu la Paroko na Msaidizi wake yaani wasio na upande wowote wa timu, `waligaragazwa' vibaya na washabiki wa Simba na Yanga kwani waliambulia sadaka `kiduchu.'

Wakati wa kukusanya sadaka hizo, walijitokeza waumini wawili na Mtawa mmoja wakasimama mbele ya Kanisa wakiwa wameshika vikapu vya kukusanyia sadaka.

Mwandishi wa habari hizi aliyekuwemo kanisani humo, alimshuhudia mmoja wa waumini akishika jezi ya rangi nyekundu na kapu jekundu ikiwa ni alama ya Simba, mwingine akishika jezi na kapu ya manjano kama utambulisho wa timu ya Wananchi (Yanga).

Hivyo, waumini ambao ni wapenzi wa Simba, walipeleka sadaka zao kwenye kapu la rangi nyekundu na wa Yanga, walitumbukiza katika kapu la rangi ya manjano.

Aidha, kapu la Paroko na Msaidizi wake, halikuwa na rangi maalum na lilishikwa na mmoja wa Watawa.

"Haya, sasa natangaza matokeo ya uchangiaji sadaka kwa Simba na Yanga. Simba wamechangia Sh……, Yanga Sh…… na Kapu la Baba Paroko na Msaidizi wake (wasio na timu), wamechangia Sh….. Kwa matokeo haya, Mayele (Yanga), ametetema, Simba na Baba Paroko pamoja na Msaidizi wake, wamedondoshwa," alitangaza mmoja wa wajumbe wa Kamati ya Walei na kulipuka kwa shangwe kanisani kutoka kwa washabiki wa upande wa Wananchi.

Hata hivyo, baada ya ibada kumalizika, mwandishi wa habari hizi aliwaona baadhi ya waumini wa pande zote wakiwa wamekaa vikundi vikundi wakipanga mikakati mizito ya kuhakikisha kwamba, Jumapili itakayofuata, wanawagaragaza wenzao wa upande mwingine.

Mfumo huo mpya wa ukusanyaji sadaka, umebuniwa kwa lengo la kuwahamasisha waumini kuwa na moyo wa kutoa sadaka zaidi kwa ajili ya maendeleo ya Parokia yao.

Utaratibu ambao hutumika mara zote, ni ule wa kupitia katika Kanda na Jumuiya zilizoundwa kila Parokia ambapo viongozi wake hufanya kazi ya ziada kuwahamasisha waumini wa maeneo yao, kutoa sadaka kwa ajili ya maendeleo ya Kanisa.

**Kutokana na asili yao, wanyama pori hawa hula nyama na hutembea kwa makundi na wakati mwingine huingia katika maeneo ya binadamu na kuua mifugo na ndipo wanapo uawa kwania ya kulipa kisasi...**

Gazeti hili la UELEKEO limepata taarifa kuwa mtindo huu wa ukusanyaji sadaka, pia umekuwa ukitumika katika baadhi ya Parokia nyingine jijini Dar es Salaam.

Mmoja wa waumini wa Parokia (jina pia limehifadhiwa), iliyoko katika Wilaya ya Ilala ambaye hakutaka jina lake litajwe, alilidokeza UELEKEO kuwa, mfumo huo wa ukusanyaji sadaka kutoka kwa waumini, hutumika pia katika Parokia hiyo kwa lengo la kuhamasisha michango ya ujenzi wa Kanisa au wakati wa harambee.

Muumini huyo alisema kwa upande wao, wamekwenda mbali zaidi kwani huandaliwa Kombe maalum kwa ajili ya kuwakabidhi washabiki wa upande wa timu inayoibuka kidedea.

"Baada ya Kombe hilo kushikiliwa na washabiki wa Yanga kwa muda mrefu, sasa washabiki wa Simba wamepindua meza na kulishikilia Kombe hilo. Lakini washabiki wa Yanga, wanazidi kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa Kombe hilo wanalirejesha mikononi mwao," alisema muumini huyo.

Baadhi ya waumini wameuelezea mfumo huu wa ukusanyaji sadaka kuwa inaonesha wazi kwamba, Kanisa linawajua washirika wake, linajua wanayoyapitia kwenye furaha na huzuni. Pia linawaonesha kuwa kama wao ni sehemu ya Kanisa maana yake hata mambo yao pia (yasiyo ya dhambi), yanaweza kuwa sehemu ya Kanisa.

Mbali ya kanisani, mtindo wa kutumia mashabiki wa timu hizo, pia umekuwa ukitumika kwenye sherehe za harusi kwa kuwaita wageni waalikwa kuwazawadia maharusi ambao lazima mmoja awe upande wa Simba na mwingine upande wa Yanga.

Utaratibu huu kwa kiasi kikubwa huwawezesha Bibi Harusi na Bwana Harusi, kujizolea zawadi `kibao' kutoka kwa washabiki wa Simba na Yanga.

**TOA MAONI YAKO KUPITIA NAMBA: 0713263775 au 0748115000**



# Wanafunzi wapigwa `stop' masomo wakituhumiwa kwa ushoga, usagaji

**Waandishi Wetu, Njombe na Dar**

WANAFUNZI 16 wa Shule ya Sekondari Yakobi iliyopo Halmashauri ya Mji wa Njombe, wamesimamishwa masomo wakituhumiwa kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Hamis Issah, alithibitisha taarifa hizo.

Hata hivyo, Kamanda Issa, alisema mchakato unaoendelea kwa sasa kuhusiana na watuhumiwa hao, ni kwa wataalamu wa afya kuwafanyia uchunguzi wa vipimo ili kubaini ukweli wa madai hayo.

Alisema tangu kuanza kwa mahojiano kati ya polisi na watuhumiwa, bado wanaendelea kuwakamata na kuwashikilia washukiwa wengine.

"Tunaendelea kuwakamata wengine wanaotajwa katika mahojiano tunayofanya,

> **Tunaendelea kuwakamata wengine wanaotajwa katika mahojiano tunayofanya, idadi ya watuhumiwa inaongezeka. Wataalamu wa Afya walikwishaanza uchunguzi wa kitabibu kubaini vitendo hivyo...**




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Hamis Issah

idadi ya watuhumiwa inaongezeka. Wataalamu wa Afya walikwishaanza uchunguzi wa kitabibu kubaini vitendo hivyo," alisema Kamanda Issah bila kutaja idadi ya wanafunzi wanaotuhumiwa kufanya vitendo hivyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Erasto Mpete, naye alilithibitishia Uelekeo kuwepo kwa taarifa hizo.

Mpete alisema jumla ya wanafunzi 16 wa kike na kiume, wanaoshikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani humo kwa tuhuma za ushoga na usagaji.

Hata hivyo, Mpete alisema taarifa za wataalamu wa afya ndizo zinazosubiriwa ili hatua zaidi zinazostahiki, zichukuliwe dhidi yao.

Aidha, amewataka wazazi kuwa makini na watoto wao kwa kuwakagua ikiwa ni pamoja na kuwalea katika mila, desturi na miongozo ya imani za dini ili kutengeneza taifa lenye maadili mema.

Baadhi ya wazazi na walezi wa wanafunzi hao ambao hawakutaka watajwe majina yao, wamethibitisha watoto wao kusimamishwa masomo na kuiomba serikali ifanye uchunguzi wa haraka kuwabaini wahusika na wale wasiohusika, warejee shuleni kuendelea na masomo.

Juhudi za kumpata Afisa Elimu Sekondari Halmashauri ya Mji wa Njombe azungumzie suala hilo, ziligonga mwamba kwani kila alipopigiwa simu yake ya mkononi, iliita bila kupokelewa.

Kadhalika, Mkuu wa shule hiyo alipopigiwa simu yake ya mkononi, pia iliendelea kuita kwa muda mrefu bila kupokelewa na siku iliyofuata, ilipokelewa na aliyejitambulisha kuwa ni Katibu Muhtasi, lakini alisema hakuwa na mamlaka ya kulizungumzia hilo.

# ...Waislamu Singida wajipanga kuandamana kupinga ushoga

**Na Claudia Kayombo, Singida**

WAISLAMU mkoani Singida, wamepanga kufanya maandamano kupinga viashiria vya ndoa za jinsia moja mkoani humu,

Sheikh wa Mkoa wa Singida, Issa Nassoro, amesema maandamano hayo yanatarajiwa kufanyika Aprili 16, mwaka huu na kutoa wito kwa Waislamu mkoani humu, kujitokeza kwa wingi wakiwa na mabango ya kulaani vitendo hivyo.

Aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na gazeti hili ofisini kwake mjini hapa hivi karibuni.

Shekh Nassoro alisema wameona ni vema wafanye maandamano ya amani kwa kuwa hawawezi kufumbia macho vitendo hivyo vya kifedhuli na kuanza kushamiri mkoani hapa.

Alifafanua kuwa maandamano hayo wanayotarajia kumuomba Mkuu wa Mkoa, Peter Serukamba, awe mgeni rasmi, wana imani yatasaidia kwa kiasi kikubwa wahusika kuachana na mipango yao hiyo miovu ya kuieneza tabia hiyo mkoani humu.

Katika Kongamano la Wanawake wa Kiislamu lililofanyika mkoani humu hivi karibuni, Sheikh Nassoro aliwahi kuonesha wasiwasi wake kuhusu baadhi ya watu kuanza kuwaharibu watoto wadogo wa kiume.

Hivyo aliwataka kinamama kujenga tabia ya kuwachunguza zaidi ili kuwabaini mapema iwapo wameanza kuwafunza vitendo hivyo kwa kuwa wao ni walezi namba moja wa watoto.

Aidha, Sheikh Nassoro alisema



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba

upo mpango wa Masheikh wa kata pamoja na yeye mwenyewe, kuomba wawe wanakwenda katika shule za msingi kutoa elimu kwa watoto kuhusu madhara ya kujiingiza katika vitendo vya mapenzi ya jinsia moja.

Alisema ana imani watoto hao wakipatiwa elimu stahiki Mapema, itasaidia kutoa taarifa mapema kwa wazazi au walezi na hivyo kuwanusuru kuzama katika lindi la mapenzi ya namna hiyo ambayo ni utamaduni wa kigeni katika Bara la Afrika.

Hata hivyo, Sheikh Nassoro wakati akisema kuna viashiria vya vitendo vya ndoa za jinsia moja, amekiri ukahaba kushamiri katika maeneo mengi mjini hapa.

"Hali mbaya kwa wanaotumia miili yao kujiuza, zamani walikuwa na sehemu maalum za kufanyia biashara hii, lakini sasa wapo katika maeneo mengi wengine wanakodi hadi nyumba kwa ajili hiyo," alisema Sheikh Nassoro.

# Kabudi ataka waathirika ubakwaji walipwe fidia

## Asema sheria inawaangalia tu wakosaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa zamani wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi, amependekeza waathirika wa uhalifu wa kijinai wakiwamo waliobakwa, walipwe fidia na kupewa ushauri wa kisaikolojia, badala ya mifumo ya hakijinai kuwatumia tu kama mashahidi mbele ya Mahakama.

Aidha, Chama cha Majaji Wastaafu (Tarja), kimetaka wakuu wa mikoa na wilaya, kupunguziwa mamlaka ya kuweka watu ndani huku kikipendekeza vifo vyenye utata vichunguzwe na Mahakama.

Profesa Kabudi ambaye pia aliwahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, alitoa mapendekezo hayo jijini Dar es Salaam jana mbele ya Tume ya Kurekebisha Mifumo ya Hakijinai inayoongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu, Mohammed Othman Chande.

Alisema kwa hali ilivyo sasa, mwathirika wa uhalifu hatazamwi sana na sheria badala yake, mifumo imemlenga zaidi mhalifu.

"Tumekazania sana kumwangalia mhalifu na adhabu kwao na kumsahau mwathirika…ni lazima sasa tuwe na mfumo wa fidia wa kuwasaidia hasa kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia, kubakwa na kudhalilishwa," alisema.

Profesa Kabudi alisema mwathirika wa uhalifu, anapaswa kusaidiwa kitabibu ili aweze kutoka kwenye tatizo alilonalo.

Alisema amependekeza pia mafunzo ya ufundi kwa wafungwa na fursa ya masomo kwa watu wanaokutwa na hatia wakiwa na umri mdogo.



Waziri wa zamani wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi.

Katika eneo hilo, amependekeza pia magereza ya wazi kwa wafungwa wataalam kama madaktari na wahandisi, ambao wametiwa hatiani kwa makosa madogo ili waendelee kufanya kazi.

Alisema amependekeza pia maboresho ya sheria nyingi mbalimbali pamoja na muundo wa taasisi zinazoshughulikia mifumo ya hakijiani likiwamo jeshi la polisi.

"Nimetoa maoni kuhusu miundo, mifumo, ajira na nini…lakini ni vizuri tukaiachia tume ichambue halafu itoe taarifa," alisema.

Profesa Kabudi alipendekeza pia kiundwe chombo kitakachosikiliza wananchi ambao wataona wamenyanyashwa na taasisi zinazosimamia hakijinai, hususani matumizi mabaya ya madaraka yanayofanywa na baadhi ya maofisa wa vyombo hivyo.

Alisema taasisi zinazoshughulikia mfumo wa hakijinai zinapaswa kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ibara za 9, 12 na 13 za Katiba, zinazosisitiza heshima na utu wa kila mtu bila kujali ni mhalifu au mwathirika wa uhalifu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Tarja, Jaji mstaafu, Thomas Mihayo, alisema wakuu wa mikoa na wilaya wamekuwa na kasumba ya kutoa amri ya kumkamata mtu hivyo wamependekeza amri hiyo isiwe kauli ya mwisho, bali mtuhumiwa apewe haki ya kumshtaki kiongozi huyo ikiwa atakamatwa kwa uonevu.

> **Tumekazania sana kumwangalia mhalifu na adhabu kwao na kumsahau mwathirika…ni lazima sasa tuwe na mfumo wa fidia wa kuwasaidia hasa kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia…**

"Tumegusia haya mamlaka ambayo wakuu wa mikoa na wilaya wanayatumia…eeh kamata watu, muweke ndani, ondoka naye n.k. Tumependekeza kwamba ili yaweze kufuatiliwa na kuwa utekelezaji wa maana, kwanza maagizo hayo yatolewe kwa maandishi ili kama mtu ataona awe na haki ya kushtaki kuwe na ushahidi," alisema.

Jaji Mihayo alisema: "Tumependekeza kuhusu hizi kamati za ulinzi na usalama, kumekuwa na kutoeleweka kwa kazi yake. Kazi yake siyo kukamata watu wala kuagiza watu kukamatwa ni kuangalia hali ya mkoa au wilaya ya kiusalama."

Alisema kamati hiyo ikibaini kuna shida ya usalama inapaswa kuwasiliana na jeshi la polisi ambalo ni mjumbe, ili kudhibiti matukio ya uhalifu na siyo vinginevyo.

### VIFO POLISI, MAGEREZA

Kuhusu vifo vyenye utata, Tarja imependekeza kuwa uchunguzi wa matukio hayo ufanywe na Mahakama ili kuondoa sintofahamu.

Alisema kulikuwa na sheria ya inquest (uchunguzi), inayotoa mamlaka ya kuchunguza sababu za kifo kwa vifo vyenye utata, akitaka ombi la uchunguzi litolewe na Hakimu au Jaji; ili kutoa haki kwa walalamikaji.

"Mtu akifariki dunia gerezani, akifia kituo cha polisi au mahali penye wasiwasi, kifo hicho kinachunguzwa na hakimu. Akijiridhisha kuna mtu anapaswa kushtakiwa basi anaagiza mtu fulani au kundi fulani wakamatwe na kushtakiwa. Hamtii mtu hatiani bali atapendekeza watuhumiwa wafunguliwe mashitaka. Hivi ndivyo ilivyokuwa huko nyuma," alisema.

Alifafanua: "Ndiyo maana unaona mtu anapofariki dunia polisi wanasema amejinyonga, ndugu wanakataa. Kama ingefanyika inquest angejulikana nani amehusika. Hakimu angefika mahali na kusema hakufa kifo cha kawaida, aliuawa au aliteswa hadi akafa."

### PLEA BARGAINING

Kuhusu plea bargaining, Jaji Mihayo amependekeza utaratibu huo utathminiwe kwa kuwa watu wanaoingia kwenye mpango huo ni wale ambao wameshanyanyaswa kwa kuwekwa mahabusu muda mrefu, hivyo wanakubali masharti ya plea bargaining ili kukwepa mazingira ya magereza.

"Plea bargaining kama ilivyo siyo haki kwa sababu haijaeleza itafanyika kwa wakati gani na haina usawa. Unakuta mtu amekaa ndani kwa kosa la uhujumu uchumi, yuko ndani miaka sita halafu anaambiwa aende kwenye plea bargaining…ana uhuru wa ku-plea bargaining huyo,?" Alihoji Jaji Mihayo.

Alisema kinachotakiwa kufanyika ni kuruhusu plea bargaining kwa uwazi badala ya kutumia utaratibu huo kuumiza watu. Kadhalika, Jaji Mihayo amependekeza Mwendesha Mashitaka wa Serikali (DPP), aondolewe mamlaka ya kunyima watuhumiwa dhamana.

"Uhuru wa mtu ni wa msingi na ni kiini cha ubinadamu na hivyo sheria yoyote inayomnyima mtu uhuru, iangaliwe kwa makini," alisema.

# Tafiti zitasaidia kutatua changamoto – SUZA

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

MKUU wa Shule ya Afya na Sayansi ya Tiba kutoka Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Salma Abdi Mahmoud, amesema taarifa za tafiti zinazofanywa na wataalamu nchini, zitasaidia kuchangia kutatua changamoto zinazowakabili watu katika jamii. Aliyaeleza hayo alipozungumza katika mafunzo ya siku tano kwa wanataaluma wa shule hiyo yanayohusu uchakataji na uchambuzi wa takwimu na uandishi wa ripoti za utafiti.

Hafla hiyo ilifanyika Chukwani, nje kidogo na mji wa Zanzibar.

Alisema, wameamua kufanya mafunzo hayo ili kuongeza uwezo katika kufanya tafiti zenye ubora na kuchangia katika maendeleo ya jamii.

Aidha, alisema mafunzo hayo pia yatasaidia kuendeleza sekta ya afya na sayansi za tiba katika shule hiyo na kwamba lengo la mafunzo hayo ni kupata kukumbushana na kupeana elimu na ujuzi wa taaluma hiyo ya utafiti.

"Lengo letu ni kuwawezesha na kuongeza uwezo katika kufanya tafiti za kisayansi na kuchangia katika maendeleo ya jamii nchini kupitia sekta ya elimu, afya na sayansi za tiba katika skuli yetu," alisema.

Hata hivyo, alisema, hali ya tafiti Chuoni humo ipo vizuri ambapo kwa miaka miwili iliyopita wameshatoa takribani ya tafiti 20 ambazo zimechapishwa katika ngazi za kimataifa. Alisema kati ya tafiti hizo zinahusu hasa maradhi ya binadamu ambazo zinaleta matokeo mbalimbali licha ya kuwa fedha za tafiti wanategemea za ndani. Naye Mkuu wa Tafiti na uandishi wa ripoti kutoka SUZA ambaye pia ni Mkufunzi wa mafunzo hayo, Dk. Chukwuma Okafor, alisema kumekuwepo na umuhimu kwa wanataaluma wote wa afya na sayansi za tiba kuwa na ujuzi wa kutosha katika eneo la kufanya tafiti ili matokeo yake yazae matunda. Alisema ni vyema wanataaluma hao kutumia fursa hiyo ya kubadilishana mawazo na uzoefu kwa kushirikiana li kuboresha uwezo na kuwa na muda wa kufanya tafiti za kimaendeleo.

Akizungumza kwa naiba ya washiriki wenzake, Shuwena Abdallah Hamad, kutoka Idara ya Uuguzi na Kinga, waliahidi kuyafanyia kazi mafunzo watakayo patiwa.

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

**HII NI KERO**



## Kumwaga mitusi hadharani

**SUALA la haki ya mtu kuzungumza hilo ni la msingi, lakini nini anazungumza, wapi na wakati gani, ni muhimu zaidi. Kumekuwa na tabia isiyo ya kistaarabu kwa miongoni mwa jamii husussan vijana, kuzungumza lugha za matusi tena kwa sauti kubwa, bila kujali kuna hadhira gani na ya rika ipi! Utamkuta kijana mwenye akili zake timamu, akiropoka mitusi ya nguoni mbele ya watu wakiwemo watoto. Upo umuhimu kwa mamlaka husika, kuwachukulia hatua za kisheria watu wa nama hii kwa kuwa kuporomosha matusi hadharani, ni kosa kisheria.**




**MAONI YA MHARIRI**

## Kamwe tusikubali ndoa za jinsia moja

KUMEKUWA na mjadala wa ndoa za jinsia moja huku baadhi ya mataifa hususan nje ya Bara la Afrika, yakipigia chapuo uovu huo. Dhana hii ya ushoga kwa ujumla wake, inagusa sana imani, maadili na misingi ya uumbaji wa wanadamu yaani mume na mke.

Vitabu vya dini vinatufundisha kuwa, Mwenyezi Mungu wakati anamuumba mwanadamu, alianza kumuumba mwanaume (Adamu), kisha akaona umuhimu wa kumpatia msaidizi wake mwanamke ambaye ni Hawa/Eva.

Na akawaambia, enendeni na mkaujaze ulimwengu, akiwaagiza Adamu na Hawa/Eva maneno hayo. Kwa mantiki hii, Mungu aliruhusu mahusiano ya jinsia mbili tofauti (mume na mke) ili kuijaza dunia na si ya jinsia moja.

Labda tujiulize, ndoa ya jinsia moja inalenga nini? Kuijaza dunia au ni kwa lengo lipi?

Ni dhana inayopingana na mahusiano ya watu wa jinsia tofauti yaani mume na mke. Urafiki wa watu wa jinsia moja, upo na ulikuwepo tangu zamani, lakini si huu wa mahusiano wa kimapenzi au wa ndoa za jinsia moja. Sasa dunia imechafuka, yanayoibuka yanaashiria machafuko na yenye asili ya shetani.

Na kwa bahati mbaya, machafuko haya yanaungwa mkono na mataifa yenye nguvu kiuchumi, kisiasa na hata kijeshi.

Dunia ingefurahi sana iwapo mataifa hayo yanayoitwa `makubwa' kama yangesimamia maendeleo makubwa ya elimu, sayansi na teknolojia badala ya kupigia chapuo ndoa za jinsia moja.

Mathalani, katika toleo letu la leo, kuna moja ya habari inayoelezea kusimamishwa masomo kwa wanafunzi wa shule moja mkoani Njombe kwa tuhuma za kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja. Bado hawajathibitika, lakini wanafanyiwa uchunguzi wa kiafya kubaini tuhuma hizo.

Sisi Uelekeo, tunapinga kwa nguvu zote dhana hii ya ndoa za jinsia moja na tunaomba Watanzania kwa ujumla wake, kamwe tusikubali kujiingiza kwenye `uasi' huo kwani mbali ya kumkosea Mwenyezi Mungu, pia ni kinyume kabisa cha maadili yetu.



## Wasiliana nasi

| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255693257410 / 0766005061 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255713055011 / 0621350860 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** jaridalamwekeleo@gmail.com |





Na Godfrey Sanga
JICHO LANGU
godfreysanga774@yahoo.com

# Tuyapige teke mapenzi ya jinsia moja

HIVI karibuni, limeibuka wimbi/janga kubwa la watu wanaotetea pia kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja maeneo kadhaa duniani,

Baadhi ya mataifa yamediriki hata kupitisha sheria inayoruhusu watu wa jinsia moja kuoana na kufunga ndoa na hivyo kuishi pamoja kama mke na mume.

Wimbi la matukio haya yameibua sintofaham kubwa kwa mataifa mengi, hasa yale yasiyokuwa na utamaduni wa kufanya hivyo hususan kwa nchi za Afrika.

Bila shaka hautakuwa mbali na mimi katika kutazama hili kwa jicho la tatu, kwani jambo hili kwa utamaduni wetu wa Kiafrika, ni kukiuka maadili. Unaweza ukajiuliza kwanini vitendo hivi vinazidi kushamiri hivi sasa?

Watetezi wa masuala ya haki za binadamu eti wanadai "kupinga ndoa za jinsia moja, ni kuikatili jamii hiyo na kuwanyima haki yao ya msingi."

Ni kweli binadamu ana haki zake za kimsingi kama vile haki ya kuishi, kusikilizwa, kuwajibika na kuzungumza pasipo kuvunja sheria, kuzitaja baadhi.

Sasa hiyo haki ya mapenzi ya jinsia moja iatoka wapi?

Ninayapongeza baadhi ya mataifa yaliyokwisha kutoa tamko la kutokukubaliana na vitendo hivyo likiwemo taifa la Kenya, Uganda na Tanzania.

> **Ninayapongeza baadhi ya mataifa yaliyokwisha kutoa tamko la kutoku kubaliana na vitendo hivyo likiwemo taifa la Kenya, Uganda na Tanzania...**

Nina imani tukishirikiana tutalipunguza janga hili kama si kulimaliza kabisa.

Pengine niseme janga hili limechangiwa na utandawazi au wazazi kusahau majukumu yao ya kutokuwa karibu na watoto wao au baadhi ya serikali kutoweka sheria kali za kudhibiti suala hili.

Jamii ya watu hao hivi sasa imejiweka wazi (hadharani) bila woga katika baadhi ya maeneo.

Ipo haja ufanyike msako mkali na wahusika wote na wanaoshabikia vitendo hivyo, washughulikiwe

Na biashara yoyote bila wateja, lazima ife, kwa msingi huo ni dhahiri inashamiri kwa sababu wateja wa biashara hii wapo.

Kuna baadhi ya mashirika yanayotengeneza watu wa jamii hiyo kwa kuangalia maslahi yao binafsi wakati wengine wanaharibikiwa.

Mamlaka husika iwajibike kuchunguza hili na yafutwe pindi yakibainika kufanya hivyo.

Vitabu vya dini na tamaduni zetu Afrika zinakataa. Imetoka wapi hii mwanaume kwa mwanaume au mwanamke kwa mwanamke wakaoana?

Dunia inaelekea wapi, inapaswa binadamu tujitathmini maana tunakoelekea hivi sasa, siko.

Serikali, viongozi wa dini, wazazi na jamii kwa jumla, tushirikiane kulipinga jambo hili, tutoe elimu yenye maonyo kwa vijana wetu ili waachane na dhana hii potofu.

# Vijana waaswa kujiunga vikundi vya ujuzi

**Na Juliana Ramadhani, Kibaha**

WAHITIMU wa vyuo vikuu na vijana wasio na ajira kwa jumla, wameshauriwa kujiunga katika vikundi kulingana na ujuzi walionao ili kazi zinapotokea, waunganishwe kwa urahisi. Ushauri huo ulitolewa na Afisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Mji wa Kibaha mkoani Pwani, Leah Lwanji, ambaye alisema hatua hiyo itasaidia kupunguza wimbi la vijana wasio na ajira nchini.

Lwanji alisema suala la vijana kukosa ajira, limekuwa likizungumziwa katika maeneo mengi nchini, lakini baadhi yao hawaelezi suluhisho nini kifanyike ili kulimaliza.

"Wapo vijana wamemaliza vyuo vikuu na hawana kazi, badala yake wameishia kuendesha bodaboda na wengine wameishia kukaa vijiweni wakiilalamikia serikali kwa kutowapatia ajira," alisema Lwanji.

Alisema hali hiyo inataka kuwaamsha vijana kwa kuwapatia nyenzo mbadala ya kujiajiri na kupatiwa elimu ya ujasiriamali ili waweze kuanzisha vikundi na kujiajiri. Kadhalika, Lwanji alisema mbali ya kuwa na fani, pia vijana wanatakiwa kuhamasika na kuunda vikundi ambavyo watapata katika halmashauri zao na kufanya shughuli mbalimbali za kijasiriamali.

> **Wapo vijana wamemaliza vyuo vikuu na hawana kazi, badala yake wameishia kuendesha bodaboda na wengine wameishia kukaa vijiweni wakiilalamikia serikali kwa kutowapatia ajira...**

Alisema yapo mashirika na taasisi zinafanya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo barabara, hivyo kukiwa na vikundi vya vijana wenye vigezo, zinapotokea fursa kama hizo, kipaumbele kitatolewa kwao.

Lwanji, alishiriki kongamano la uwasilishaji wa utafiti wa vijana kuhusiana na utekelezaji wa Lengo Namba 16.7.2 la Malengo ya Maendeleo Endelevu Tanzania.

Utafiti huo uliofanywa katika halmashauri 18 nchini zinazotekeleza mradi wa Kijana Wajibika ikiwemo Taasisi ya Pwani Youth Network.

Taasisi ya Pwani Youth Network, ilishiriki utafiti huo kwa Kibaha Mji na iliandaa kongamano hilo kwa lengo la kujadiliana na vijana na viongozi wa serikali kuhusiana na yaliyobainika.

Kwa mujibu wa Lwanji, ni wakati mwafaka sasa kwa vijana kutambua fursa zilizopo na kuzitumia kwa kuunda vikundi ambavyo vitakavyowaunganisha na kazi zinazopatikana, lakini pia kunufaika na mikopo ya halmashauri.

"Hamasikeni kuunda vikundi na mvisajili tuwatambulishe mpate kazi, matokeo ya huu utafiti, umeibua masuala yanayohusu vijana kisiasa na kiuchumi na hii inataka pia vijana washiriki wanaposhirikishwa kuondoa vikwazo vilivyopo kwenye maeneo yao," alisistiza Lwanji.

Mkurugenzi wa Pwani Youth Network, Fred Mtei, kwa upande wake alisema katika utafiti huo, ulibaini mifumo inayotumika kutoa taarifa ni kikwazo kwa vijana kushiriki mikutano na shughuli mbalimbali.

Mtei alisema kutokana na hali hiyo, taasisi yao ina wajibu wa kutoa elimu kwa vijana kushiriki mikutano kwenye maeneo yao ili kujua kinachojadiliwa na mipango inayowekwa.

"Wito wangu taasisi za kiraia, tushirikishe jamii na serikali kuhakikisha fursa zinawafikia wananchi sisi tuwe kiunganishi, kwa kufanya hivi tutafikia malengo ya maendeleo," alisema Mtei.

Mmoja wa vijana walioshiriki katika kongamano hilo la kupokea matokeo ya utafiti, Ruth Macha, alisema ushiriki wa vijana wa kike kwenye mambo mbalimbali ikiwemo ya uongozi, bado ni mdogo na kwamba wengi wao wameshindwa kuthubutu kutokana na hofu, jambo ambalo linahitaji elimu.

# `Wakulima tumieni mbolea ya Kiwanda cha Dodoma'

**Na Claudia Kayombo**

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewataka wakulima nchini kutumia mbolea ya kiwanda kipya cha Dodoma ili kuzalisha mazao yenye tija kwa jamii na taifa.

Amesema mbolea hiyo isiyo na kemikali ya kudhuru udongo, ni nzuri kupandia, kunenepesha na kukuzia mimea, hivyo waitumie kwa mazao yote. Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki mkoani hapa wakati akihitimisha hotuba yake katika hafla ya uzinduzi wa kampeni ya `Kijanisha Maisha' iliyozinduliwa na Taasisi ya Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (PASS Trust).

"Ndugu zangu, kilimo ni uhai wetu na kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa taifa letu, hivyo ni lazima tukilinde kupitia ubunifu mbalimbali hasa kuchukua hatua zinazokabiliana na mabadiliko ya tabianchi," alisema na kuongeza:

"PASS wameonesha njia, tuwaungeni mkono kupitia shughuli zetu ili kesho ya kilimo chetu, kesho ya maisha yetu iendelee kuwa bora zaidi. Bila kufanya hivyo, athari za mabadiliko ya tabianchi zitaathiri maendeleo ya kilimo."

Alisema: "Kupitia hafla hii, nataka niwashawishi wakulima Singida na Watanzania kwa jumla, tumepata bahati kujengewa kiwanda cha mbolea



**Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua shehena ya mbolea alipotembelea Kiwanda cha Mbolea cha Itracom cha Nala jijini Dodoma, mwishoni mwa mwaka jana. Wa tano kushoto, ni Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kushoto ni Mwekezaji wa kiwanda hicho, Ntigacika Adrean na wa pili kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda, Nduwimana Nazaire.**

Dodoma, nimeambiwa hapa Singida wataweka tawi lao pia, itumieni kwa mazao yote, nina uhakika tukitumia mbolea hii ambayo ni rafiki kwa udongo kama sisi Singida karibu na Dodoma uzalishaji wa mazao mwakani, utakuwa wenye tija kubwa."

Serukamba alizipongeza taasisi za fedha za mkoani Singida kwa mchango zinaoutoa katika sekta ya kilimo, kwa kuunga mkono maagizo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kupunguza riba katika mikopo ya kilimo kwa hadi asilimia tisa. "Benki zote zilizounga mkono agizo hili, nazipongeza sana na natoa wito kwa benki zote kufuata uelekeo huu ili tuondoe maumivu kwa wakulima," alisema.

Aidha, aliwaomba wadau wa kilimo kuendelea kufanya shughuli za uzalishaji kwa kuzingatia kanuni za ukuaji wa Kijani Shirikishi kama ambavyo PASS Trust wanasihi ili kutunza mazingira huku tukizalisha kwa tija," alisema. Kwa upande wake, Meneja wa Maendeleo ya Biashara wa PASS Trust, Herman Bashiri, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, alisema taasisi yake ina mchango mkubwa katika kuchochea na kuwezesha ukuaji wa kilimo nchini huku ikitoa kipaumbele kwa vijana na wanawake ambapo inawapa dhamana ya mikopo na huduma za maendeleo ya biashara ili

# CWT yapiga jeki mil. 10/- Tuzo za Elimu Ruangwa

**Na Abdul Mitumba, Ruangwa**

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimetoa Sh. milioni 10 kufanikisha Tuzo mpya za Elimu wilayani Ruangwa ambapo wanafunzi wa darasa la saba, vidato vya pili, nne na sita wa mwaka jana waliofanya vizuri kutoka katika shule za wilayani humu, wametuzwa.

Katika tuzo hizo, walimu wa shule za msingi na sekondari zilizofanya vizuri,

pia wametuzwa na kwamba hatua hiyo imelenga kuinua ari ya ufundishaji kwa walimu na kujifunza na kujisoma kwa bidii kwa wanafunzi ili kufikia malengo ya Mkoa wa Lindi ya ufaulu wa asilimia 100.

Kwa sasa Wilaya ya Ruangwa imefikisha asilimia 98 kiwango cha ufaulu kwa shule zake za msingi na sekondari, hivyo kushika nafasi ya kwanza kati ya Halmashauri sita za Wilaya za Mkoa wa Lindi na ya 19 kitaifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Frank Chonya, alisema kwa kutoa kiasi hicho, CWT imekuwa taasisi ya elimu iliyochangia fedha nyingi zaidi katika kufanikisha tuzo hizo.

"Wadau wengine waliochangia kufanikisha tuzo hizo ni pamoja na Mohamed Dewji (MO) aliyechangia Sh. milioni tano, Kikundi cha Wachimbaji wadogo wa madini Namungo Sh. milioni tatu na mfanyabiashara wa Ruangwa, Shaban Saidi, aliyechangia Sh. milioni moja," alifafanua. Katibu wa CWT Wilaya ya Ruangwa, Kabarata, alithibitisha chama chake kuchangia na akasema tukio lolote linalohusu elimu, chama chake kinahusika moja kwa moja.

"Ni vigumu CWT kuitenganisha na tuzo za elimu, maana ndiyo eneo lake la

kujidai na hasa ikizingatiwa wanaolengwa kutuzwa na walimu na wanafunzi ambao wanafundishwa na walimu," alisema Kabarata.

Wanafunzi waliotuzwa ni wale waliopata alama za madaraja ya A, B na C kwa kila somo, ambapo kwa wanafunzi wa shule za msingi kila somo limelipwa

kati ya Sh. 3,000 na 10,000 kwa masomo ya sanaa na sayansi wakati kwa sekondari kila somo la sayansi lililopata alama A limetuzwa Sh, 10,000.

Ama kwa upande wa shule, iliyoshika nafasi ya kwanza imetuzwa Sh.100,000, ya pili Sh.70,000 na ya tatu imepewa Sh. 50,000. Hivyo hivyo ni kwa shule zote za msingi na sekondari.

# Wanakijiji `wapagawa' kwa kupata umeme tangu uhuru

**Na Henrick Idawa, Njombe**

MAMIA ya wakazi wa Kijiji cha Mfereke, Kata ya Utalingolo, Halmashauri ya Mji wa Njombe, wameondokana na adha ya kukosa umeme tangu nchi kupata uhuru mwaka 1961.

Hatua ya awali, nishati hiyo imefikishwa katika Kanisa Katoliki Mfereke lilipo kijijini hapo.

Wakazi wa kijiji hicho, Walter Mwanyika, Juliana Mlowe na Flouris Mwanyika, kwa niaba ya wenzao, wameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwafikishia umeme kwa mara ya kwanza tangu nchi ipate uhuru.

Hata hivyo, wanakijiji hao wameiomba serikali kuifikisha haraka nishati hiyo kwenye makazi ya wananchi baada ya hatua hii ya awali ya kifikisha katika Kanisa Katoliki la Mfereke.

Aidha, wanakijiji hao wameliomba Shirika la Umeme nchini (Tanesco), kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna bora ya matumizi ya nishati hiyo.

"Kwa kweli tunamshukuru Rais Dk. Samia kwa kutukumbuka na sisi wanyonge wa kijiji hiki cha Mfereke.

> **Kwa kweli tunamshukuru Rais Dk. Samia kwa kutukumbuka na sisi wanyonge wa kijiji hiki cha Mfereke. Leo hii umeme unawaka, tunauona, kwetu ni historia kwa sababu tumekuwa tukiuona nje kabisa ya kijiji hiki...**

Leo hii umeme unawake, tunauona, kwetu ni historia kwa sababu tumekuwa tukiuona nje kabisa ya kijiji hiki," alisema Walter Mwanyika.

Naye Diwani wa Kata ya Utalingolo, Erasto Mpete, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, aliwataka wananchi kujiongeza kiuchumi kupitia nishati hiyo. Aidha, Diwani Mpete, alimshukuru Rais Dk. Samia pamoja na Mbunge wao, Deo Mwanyika, kwa hatua hiyo.

"Nishati hii ikawe chachu ya kufungua viwanda vidogo vidogo na miaka miwili mitatu ijayo, ninaamini tutaona matunda ya kiuchumi kuongezeka miongoni mwetu, ahsante Mheshiwa Rais Dk. Samia, hakika wewe ni jembe, Mheshimiwa Mbunge tusaidiane kuhakikisha kila mwananchi anapata haki ya kuingiza umeme kwa gharama elekezi," alisema diwani huyo.

Mhandisi Mkuu wa Tanesco Mkoa wa Njombe, Meshack Laurent, alielezea faida za umeme pindi utakapowafikia hadi majumbani mwao na kuwataka kuwa makini na matumizi yake na kulinda miundombinu.

Aidha, kwa upande wake, Afisa Uhusiano wa Tanesco Mkoa wa Njombe, Neema Lyakurwa, aliwataka wananchi wa Mfereke kuwa makini na vishoka watakaowafuata kutaka kuwaunganishia umeme kinyemela ndani ya nyumba zao.

"Jiepusheni na vishoka, zingatieni taratibu, wezi ni wengi na ukiona au kusikia uwepo wa watu hao, tupeni taarifa ili washughulikiwe," alisema Ofisa Uhusiano huyo.

Kijiji cha Mfereke kilichopo umbali wa takribani kilomita sita kutoka mjini Njombe, kilikosa umeme kwa miaka mingi huku vijiji vingine vya Kata ya Utalingolo kikiwemo Utalingolo, kilipata nishati hiyo kipindi kirefu.

# Askofu awaasa viongozi wa siasa kuwa wanyenyekevu

**Na Claudia Kayombo, Singida**

ASKOFU wa Jimbo Katoliki la Singida, Mhashamu Edward Mapunda, amewaasa viongozi wa siasa nchini kuacha kiburi na badala yake wawe wanyenyekevu na watii kwa wanaowatumikia ili amani iendelee kutamalaki nchini.

Amesema mataifa mbalimbali duniani, yapo katika mtafaruku unaowafanya watu wake wakose hata muda wa kujumuika katika ibada kwa sababu viongozi wao wamekosa fadhila ya unyenyekevu na utii.

Mhashamu Mapunda alitoa kauli hiyo nje ya Kanisa Kuu la Kiaskofu la Moyo Mtakatifu wa Yesu jimboni hapa kabla ya kuanza maandamano ya Sikukuu ya Matawi ikiwa ni mwanzo wa Juma Kuu la

Pasaka iliyoadhimishwa Jumapili iliyopita.

"Tuyaombee mataifa ambayo yanashindwa kuadhimisha siku hii kwa sababu hakuna amani, ni vema viongozi wetu wa kisiasa, wajifunze kwa Kristo upole na unyenyekevu," alisema Askofu Mapunda. "Wakati Yesu anaingia Yerusalemu, alipanda punda na si farasi kama walivyokuwa wakifanya viongozi au wafalme wa Kiyahudi, wengi walidhani Kristo atakuja kama kiongozi wa kidunia.

Alipanda mwana-punda, punda ni mnyama wa amani, ndugu zangu tukitaka amani tuungane na Kristo wakati huu tuteseke naye na kufufuka naye," alisema.

Alifafanua kuwa upole na unyenyekevu, ni mzizi wa fadhila zote, na kwamba jambo lolote lenye mafanikio, chanzo chake ni unyenyekevu.

Mhashamu Mapunda alisema kiongozi anayeishi maisha ya utii na unyenyekevu, Yesu Kristo ambaye katika juma hili kuu, Wakristo nchini wanaungana na wenzao duniani kukumbuka mateso, kifo na ufufuko wake, anamwezesha kuongoza kwa maadili mema na maarifa.

"Leo tunaanza Juma Kuu, tuungane na Kristo kumpa Mungu utukufu, tusafiri naye, tuteseke naye, tufe naye na kisha kufufuka naye, hakuna mwingine anayeweza kuleta amani ya kweli duniani isipokuwa Kristo Yesu Msulubiwa," alisisitiza na kuongeza:

"Hatuwezi kusema tumefufuka naye kama hatutateseka naye, Juma Kuu ni kwa ajili ya wokovu na uzima wetu, tunahitaji Juma Kuu ili tukombolewe."

Pia alisema unyenyekevu ni dira ya kiongozi wa kada yoyote iwe wa kidini au serikali, hali kadhalika, hata wazazi; baba na mama katika familia.

"Uwe Padri au Askofu, uwe Sista au Mtawa, lazima uwe mnyenyekevu, kinyume chake hutafanikiwa katika njia zako," alisema na kuongeza:

"Kinamama, kuweni watii na wanyenyekevu, kinababa kuweni wanyenyekevu, uwe sista mkuu, padre mkuu ama wewe ni baba au mama wa familia, kuwa mpole na mnyekevu katika malezi ya familia, utafanikiwa katika kila unalofanya.



**ASKOFU wa Jimbo Katoliki la Singida, Mhashamu Edward Mapunda**



**Waziri wa Maji, Juma Aweso**

# Mradi wa maji wa bil. 5.4/- wasuasua

**Na Mwandishi Wetu, Njombe**

WANANCHI wa Kata za Luponde, Uwemba na Matola Halmashauri ya Mji wa Njombe mkoani Njombe, wamelalamikia kucheleweshwa kwa ujenzi wa mradi wa maji wa Igongwi wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 5.4.

Hali hiyo inawasababisha wananchi hao waendelee kufuata huduma hiyo masafa marefu ama kulazimika kutumia maji ya mabondeni ambayo si salama.

Kwa mujibu wa ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2020/2021, ilibaini kuwapo kwa ucheleweshwaji wa utekelezaji wa miradi 18 ya maji nchini katika mamlaka za serikali za mitaa 15 yenye thamani ya Sh. bilioni 30.52 ukiwemo mradi huo wa Igongwi Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Mradi huo ulianza kutekelezwa miaka mitatu iliyopita na kusimama baada ya kile kinachotajwa kukosekana kwa fedha na kusababisha adha kubwa kwa wananchi wa vijiji vya Njomlole, Luponde, Madobole na Uwemba.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Luponde walisema wanashangazwa na ahadi za muda mrefu za kukamilishwa kwa mradi huo wa maji pasipokuwa mafanikio, jambo ambalo limekuwa kero kubwa kwao.

Mmoja wa wanakijiji hao, Pepetua Kabelege, alisema kwa sasa wanategemea maji ya kutoka mabondeni ambayo si salama.

Mkazi mwingine, Regnald Mligo, alisema baadhi yao huugua ugonjwa wa matumbo kutokana na kutumia maji hayo machafu na yasiyo salama kwa matumizi ya binadamu.

Daktari wa Zahanati ya Kijiji cha Luponde, Ibrahim Kowero, alikiri kuwapo kwa watu wanaofika hapo wakisumbuliwa na ugonjwa wa matumbo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Luponde, Fredolin Mwalongo, alisema mara kadhaa alifuatilia kwenye mamlaka husika juu ya ujenzi wa mradi huo wa maji, lakini hutolewa ahadi za kuukamilisha mradi huo zisizo na mafanikio.

Kwa upande wake, Meneja wa Wakala wa Maji na Safi wa Mazingira (Ruwasa) Mkoa wa Njombe, Mhandisi Sadick Chaka, alikiri kuchelewa kwa mradi huo akisema inatokana na sababu mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa fedha.

Hata hivyo, Mhandisi Chaka alisema kwa sasa wakandarasi wanatarajia kuingia kwenye eneo la mradi kuendelea kuutekeleza.

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu kuu

Jumatano Aprili 5 - 11, 2023




**Jarida hili haliuzwi**



# Tanzania katika sura ya pekee kwenye ramani ya diplomasia



## Dhana kuwa limau huathiri mbegu za kiume ina ukweli?

UK. 11


## M'kiti wa Serikali ya Mtaa anayefanya maajabu

UK. 14



Afya

# Dalili za ugonjwa wa gout, tiba na namna ya kujikinga




WATU wengi hususan wa rika ya kati na wazee, husumbuliwa na maumivu ya viungo vya mwili hasa magoti na vifundo vya miguu na mikono.

Baadhi hufikia hatua ya hata kuhsindwa kutembea ama kutembea kwa shida na ukiwauliza watakwambia wanasumbuliwa na ugonjwa wa Gout.

Chanzo cha maradhi haya, inaelezwa kuwa ni ulaji wa nyama nyekundu na unywaji wa pombe hasa bia. Hivyo, baadhi ya watu huuita ni ugonjwa wa watu wenye vipato vizuri kwa vile anakuwa ana uwezo wa kula nyama na kunywa bia mara kwa mara ambavyo kimsingi, huhitaji fedha na nadra kwa mtu wa kipato cha chini kuvimudu.

**GOUT NI NINI?**

Gout ni aina ya ugonjwa wa yabisi inayosababisha maumivu ya ghafla, uvimbe, wekundu na uchungu katika moja ya kiungo ama zaidi, mara nyingi kidole kikubwa cha mguuni.

> **Baadhi ya watu hushindwa kushughulikia dalili za gout. Wengine wanaweza kupatwa na ugonjwa huo mara kadhaa kwa mwaka...**

Mshauri wa Rhematologist – Gout Dk. Mohammad Irfan, anaeleza kuwa, maumivu ya ugonjwa huu hususan katika viungo, husababisha hata uzito wa shuka kwenye kiungo kilichoathiriwa, humfanya muathirika kujisikia vibaya.

**Dalili za gout**

Dalili na viashiria vya gout kwa kawaida, huanza ghafla na mara nyingi usiku.

Gout mara nyingi huhusishwa na kidole kikubwa, lakini pia inaweza kuathiri kiungo chochote mwilini ikiwemo kwenye vifundo, magoti, viwiko, viganja vya mikono na vidole.

Gout isiyotibiwa, inaweza kusababisha kuongezeka kwa usumbufu na uharibifu wa viungo.



**Dalili za gout**

Homa na kiungo kilichoathiriwa kuwa na joto.

**Sababu za gout**

Wengi huamini kwamba ulaji wa nyama nyekundu hasa ta nyama ya mbuzi na unywaji wa pombe, huchochea ugonjwa wa gout.

Pamoja na imani hiyo, lakini kitaalamu gout hutokea wakati fuwele za urate zinapokusanyika kwenye viungo vya mwili na kusababisha kuvimba na maumivu makali.

Ikiwa damu ina asidi ya uric nyingi, huunda fuwele za urea. Wakati mwili unapovunja purines ambazo ni kemikali zinazopatikana katika mwili wa binadamu, asidi ya uric huzalishwa.

Purines pia inaweza kupatikana katika baadhi ya vyakula ikiwemo nyama nyekundu na nyama yenye viungo kama ini. Baadhi ya vyakula vyenye purine ni dagaa, lakini kiasi kikubwa cha asidi ya mkojo, hukuzwa na vileo husussan bia na vinywaji vilivyotiwa sukari ya matunda (fructose).

Asidi ya uric, huyeyuka katika damu na kutiririka kupitia figo hadi kwenye mkojo katika hali ya kawaida.

Hata hivyo, mwili unaweza kutengeneza asidi ya mkojo nyingi au figo zinaweza kuondoa asidi ya mkojo kidogo wakati fulani.

Asidi ya mkojo inaweza kujikusanya kwenye viungo au tishu zinazozunguka na kutoa fuwele za urati zenye ncha kali kama sindano ambazo husababisha maumivu, kuvimba na uvimbe.

**Sababu za hatari za Gout**

Kuna mambo mengi yanayoweza kuongeza dalili za gout.

**Chakula**

Ulaji wa chakula chenye nyama nyekundu na dagaa na unywaji wa pombe hasa bia na vyenye sukari ya matunda (fructose), huongeza viwango vya asidi ya uric.

**Matatizo**

Baadhi ya watu hushindwa kushughulikia dalili za gout. Wengine wanaweza kupatwa na ugonjwa huo mara kadhaa kwa mwaka. Kwa wale walio na gout ya mara kwa mara, dawa zinaweza kusaidia kuzuia matukio. Gout, ikiwa haijatibiwa, inaweza kusababisha mmomonyoko wa viungo na gout isiyotibika.

**Tiba ya Gout**

Dawa za gout zimegawanywa katika makundi mawili. Kundi la kwanza husaidia kupunguza maumivu na uvimbe.

Aina ya pili, hupunguza wingi wa asidi ya mkojo katika damu ambayo husaidia kuzuia matatizo ya gout.

Mara kwa mara na ukubwa wa dalili na masuala mengine yoyote ya afya,ndiyo yatakayoamua ni dawa ya gani inayofaa.

**Masharti kwa watu wenye Gout.**

Mtu aliye na gout lazima afuate mambo ya kufanya.

. Kunywa maji mengi
. Weka uzito wenye afya
. Kulala vizuri kwa saa nane
. Kuepuka vyakula ambavyo vinasababisha mlipuko wa gout kama kula nyama nyekundu, kunywa pombe hasa bia.
. Kula kwa wingi mboga mboga
. Kula machungwa.

Afya



# Dhana kuwa limau huathiri mbegu za kiume ina ukweli?

LIMAU, ni miongoni mwa matunda au viungo rafiki vya mboga baadhi ya wengine wakilitumia kama dawa kulingana na maeneo husika.

Aidha, limau lilijibebea umaarufu mkubwa kipindi cha Uviko 19 kutokana na kuwa na utajiri mkubwa wa vitamini C ambayo ilionekana kuwa kinga dhidi ya ugonjwa huo.

Kauli ya watalaam wa afya

Madaktari wanasema limau ni moja ya tunda muhimu kwa mwili wa binadamu kutokana na kuwa na virutubisho vingi.

Jarida la Healthline lililoangazia kwa kina umuhimu wa limau kwa afya, linaeleza kuwa limau lina madini ya vitamin C,inayochangia kwa asilimia 20 ya mahitaji ya binadamu mwilini.

Pia limau lina utajiri wa madini ya chuma, calcium, vitamin B, potasium na magnesium.

Utafiti unaonesha kwamba, kunywa juisi ya limau, huimarisha kinga ya mwili, hupunguza hatari ya kupata magonjwa ya moyo na figo na pia huimarisha afya ya ngozi.

Hata hivyo, baadhi ya watu huamini kwamba kunywa maji ya limau ni hatari kwa maisha yao ya ndoa kwa dhana kwamba maji hayo huathiri mbegu za kiume.

Wanaamini kuwa kunywa maji ya limau, hupunguza ashiki/hisia kwa wanaume.

Lakini, wakati wengine wakiwa na dhana hiyo, baadhi huamini kwamba limau husaidia katika ukuzaji wa nguvu za kiume.

"Baadhi ya watu, hufikiria ni hatari kwa wanandoa kutumia limau, lakini hiyo ni dhana potofu. Kwa sababu utafiti unaonesha kuwa matumizi kiasi ya limau, husaidia kuimarisha nguvu za kiume," Jarida la Healthline limefafanua na kuongeza:

"Kiwango kidogo cha maji ya limau kikiwekwa katika maji ya kunywa ama kwenye chai, hakiwezi kuathiri nguvu za kiume, bali kinatengeneza na kuziimarisha zaidi mbegu na kuongeza umakini wa mishipa kufunguka."

Lakini, Jarida la Healthline linafafanua, kunywa maji mengi ya limau ni hatari pia, ila ni muhimu kwa wale wanaotaka kudhibiti ukuzaji wa nguvu za kiume kwa wale ambao hawataki tena kupata watoto kwa muda wa kushiriki tendo.

Pia, utafiti uliofanywa nchini Australia, umeonesha kuwa, kunywa maji ya limau kwa wingi, kunaweza kuathiri nguvu za kiume kwa dakika chache kabla ya tendo la ndoa.

"Endapo utatumia maji ya limau dakika 30 kabla ya kufanya tendo la ndoa, bila shaka nguvu zitaathirika," Jarida hilo linaeleza na kuongeza:

"Unashauriwa kutumia saa moja kabla ya tendo la ndoa ili lisiathiri mipango yako ya kutumia kama dawa na kuhitaji matokeo yenye umuhimu kama kupata watoto."

Kwa mujibu wa jarida hilo, haitakiwi kunywa maji mengi ya limau kwa wakati mmoja, kama inavyoelezwa kitu chochote kikizidishwa, si salama, lakini siyo kibaya kwa matumizi kidogo ya wanandoa.

Madaktari wanashauri ikiwa unataka kutumia limau nyakati za asubuhi baada ya kuamka, ukate kipande kidogo na kukiloweka ndani ya maji ya moto ama chai kisha unywe baadaye.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO): "Ni vyema kutumia limau kwenye maji badala ya kuweka kwenye kahawa ili kuepuesha utengenezaji wa asidi kwa mchanganyo huo, kwa sababu chembe chembe za limau ambazo hazijasagika, huondoa kemikali mwilini kupitia mkojo endapo utatumia katika maji."

> **Ni vyema kutumia limau kwenye maji badala ya kuweka kwenye kahawa ili kuepuesha utengenezaji wa asidi kwa mchanganyo huo, kwa sababu chembe chembe za limau ambazo hazijasagika...**

Kwa upande wake, Daktari Bingwa wa Magonjwa wa Wanawake katika Hospitali ya Consolata Father's Ikonda Wilaya ya Makete mkoani Njombe, Dk. Remegius Kayombo, akizungumza na Uelekeo kwa njia ya simu, anasema kwa jumla limau ni salama kwa watu wengi isipokuwa kuna mambo machache ya kuzingatia kwa watumiaji wa maji yake kwani athari zinaweza kutokea tangu kwenye utunzaji wa limau lenyewe.

"Athari katika limau haianzii katika unywaji wa juisi yake, bali huanzia katika utunzaji, limau ili liwe dawa nzuri, halitakiwi kupigwa na jua kwa muda mrefu tangu kuchumwa na si vema likahifadhiwa popote likiwa limetolewa ngozi yake ya nje inaweza kuwa kijani au njano," anafafanua Dk. Kayombo.

Anaongeza kuwa utafiti wa mwaka 2019, unapendekeza kwamba, juisi ya limau itumike kwa maisha ya kwani huchelewesha mabadiliko yanayohusiana na umri kwenye utumbo katika usagaji, pamoja na mabadiliko katika kuondoa bakteria wasio na faida kwenye utumbo.

Anaeleza kuwa limau likiongezwa kwenye maji, litasalia mwilini, hali ambayo itakuwa na manufaa kwa mwili.

Dk. Kayombo pia anapendekeza kuwa kunywa maji ya limau asubuhi mbali na kutumia kwenye samaki, nyama au kutengeneza saladi.

Manufaa zaidi ya limau kwa mwili

Kuna aina tofauti ya limau, lakini yaliyo maarufu ni yale malimau madogo yenye uchachu maalum na wenye kutamanisha, mengi yakipatikana barani Afrika na Asia.

.Juisi ya limau huua viini vya bakteria na huondoa harufu mbaya mdomoni.

.Juisi ya limau husaidia kutibu mafua na muwasho wa kooni.

.Maji ya limau pia yanapunguza kwa kiwango kikubwa uzani wa mwili.

.Juisi ya limau husaidia kutibu mafua na mwasho kooni.

Limau lina virutubisho muhimu kama vile madini ya vitamin C, Potasium na Magnesium. Na linatumiwa kwa njia tofauti.

Wataalamu wa afya wanasema kwamba limau lina manufaa mengi kwa mwili wa binadamu, lakini pia halikosi kuwa na madhara hata kidogo hasa kwa wale walio na vidonda vya tumbo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyowahi kutolewa na wataalamu wa lishe bora katika mashirika jumuishi yanayohusu afya makini ya binadamu, kutumia limau kunategemea afya ya mtu kwa sababu kitu chochote ambacho ni kizuri kwa mtu mmoja, huenda kikawa na madhara kwa mwingine.

Ikumbukwe kwamba kuna watu ambao miili yao inachagua vyakula, tusishangae kuona wanapata usumbufu hata wakitumia limau.

Kuna wale ambao wakitumia juisi ya limau, hutapika na wengine hupata kiungulia, kwa mujibu wa data za Jarida la Afya la Healthline.

Siasa

# ZIARA YA HARRIS KA

# Tanzania katika sura y kwenye ramani ya dipl

**Na Mwandishi Wetu**

WIKI iliyopita, Tanzania ilipokea ugeni mzito kutoka taifa maarufu zaidi duniani, Marekani; kwa kutembelewa na kiongozi anayeshika ofisi namba mbili, Makamu wa Rais wa Taifa hilo, Kamala Harris.

Wachambuzi wa masuala ya kidiplomasia, wanaitazama ziara hiyo kama nyenzo ya kukuza mahusiano yaliyopo baina ya Tanzania na Marekani, dola kubwa kiuchumi duniani.

Wanaeleza kuwa ziara hiyo ni mwendelezo unaoimarisha mahusiano ya mataifa haya mawili yenye haiba tofauti za kiuchumi na kisiasa.

Licha ya kuwa taifa dogo kiuchumi, Tanzania inaendelea kuwa mshirika mkubwa wa Marekani hasa kwa kuwa na utulivu wa kisiasa barani Afrika, sababu inayoivutia Marekani kuisogelea zaidi ikilenga kupenyeza ushawishi wake kwenye mataifa mengine barani humu.

Kamala hajaonyesha bayana azma ya ziara kuanzia Ghana, Tanzania na kisha Zambia.

Kwa Tanzania, wachambuzi wanaeleza kuwa imejikita zaidi kuimarisha urafiki kutokana na ushawishi wa Tanzania barani Afrika na katika mataifa makubwa kama China, India na Urusi, ambayo yana mahusiano mazuri na Tanzania.

Aidha, ujio wa mwanamama Kamala, huwezi kuutenga na R4 za Rais wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, ambazo zimefanikisha kuunganisha nchi, kuvutia uwekezaji na kufungua sekta nyingi za biashara.

R nne anazozisimamia ni Reconciliation (Maridhiano), Resiliency (Ustahamilivu), Reforms (Mabadiliko) na Rebuilding (Kujenga Upya).

Pamoja na mijadala inayoendelea kwenye mitandao ya kijamii kuhusu masuala ya ushoga, ujio wa Makamu wa Rais wa Marekani, ni tangazo muhimu kwenye ramani ya diplomasia kwamba Tanzania ni kisiwa chenye 'ladha' ya kipekee kwenye nyanja za demokrasia, ulinzi na usalama, uwekezaji na usawa wa kijinsia.

Tangazo hilo linakwenda mbali zaidi hadi kwenye uboreshaji wa huduma muhimu za kijamii kama afya, elimu na miundombinu.

Hii ni kwa sababu Marekani ni nchi inayojulikana zaidi kwa misingi yake ya kidemokrasia na kuheshimu uhuru wa kutoa maoni wa kila mtu; na dhana yake ya kukabiliana na magonjwa ya malaria, Ukimwi, kifua kikuu na kutoa chanjo za magonjwa mbalimbali. Haya ni maradhi yanayozisumbua nchi nyingi za Afrika.

Ujio wa Kamala una nguvu kubwa ya kubadilisha mtazamo wa jumuiya za kimataifa kwa Tanzania kabla ya Dk. Samia kuingia madarakani, ambao haukuwa mzuri kutokana na kuzuiwa kwa mikutano ya kisiasa, kufungwa kwa baadhi ya vyombo vya habari na vyombo vya dola kuwatia mikononi wakosoaji wa serikali hususani wale wa vyama vya upinzani.

Kamala amekuja nchini miezi mitatu tangu Dk. Samia aliporuhusu mikutano ya hadhara na kutangaza dhamira ya serikali yake kukwamua mchakato wa marekebisho ya Katiba, uliokwama kwa zaidi ya miaka nane tangu mwaka 2014.

Ruhusa ya mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa iliyokuwa imezuiwa kwa miaka saba tangu mwaka 2015 na dhamira ya kukwamua mchakato wa Katiba; ni mambo mawili makubwa yanayokoleza sura ya Tanzania kwenye ramani ya diplomasia.

Hatua za maridhiano kwa vitendo, zinazochukuliwa na Rais Samia kiasi cha kuongea na wananchi kupitia jukwaa la wanawake wa chama cha upinzani-Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Machi 8, ni mambo ambayo kamwe hayawezi kuinyamazisha dunia inayozungumzia amani na ustawi wa demokrasia.

"Hii ni haki kwa sheria zetu, ni haki kwa vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara, uwepo wangu leo mbele yenu ni kuja kutangaza, lile tangazo la kuzuia mikutano ya hadhara sasa linaondoka," alisema Rais Samia mapema Januari, mwaka huu.

Aliongeza: "Lakini ndugu zangu tuna wajibu, wajibu wetu serikali ni kulinda mikutano ya vyama vya siasa, wajibu wenu vyama vya siasa ni kufuata sheria na kanuni zinavyosema, twendeni tukafanye siasa za kistaarabu, tukafanye siasa za kupevuka, tukafanyeni siasa za kujenga sio za kubomoa, si kurudi nyuma hapa tulipofika. Sisi ndani ya CCM tunaamini katika kukosolewa na kujikosoa."

Kabla ya kuruhusu mikutano ya hadhara, Rais Samia aliunda kikosi ambacho kilileta mapendekezo tisa; makubwa matatu ni kuruhusiwa kwa mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, mchakato wa Katiba mpya na marekebisho ya sheria mbalimbali.

Katika hilo, alitaka kuunganisha nchi na ndiyo maana imekuwa rahisi kwake kwenda kwenye jukwaa la wanawake wa

**CHADEMA**

Kwa hiyo, Kamala amekuja nchini kipindi ambacho mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa imefunguliwa na michakato ya marekebisho ya sheria ikiendelea.

Miongoni mwa sheria zinazolalamikiwa ni ya huduma za vyombo vya habari ya mwaka 2016.



**Rais Mstaafu wa Marekani Barack Obama wa Marekani na Rais Mstaafu Rais Jakaka Kikwete akimsindikiza kupanda ndege mara baada ya kumaliza ziara yake nchini. Nyuma yao (kulia), ni Michelle Obama na Mama Salma Kikwete**

**Matatizo yanayofanana Ghana, Zambia**

Miongoni mwa mataifa aliyoyatembelea mwanamama Harris, ni Ghana na Zambia, ambayo yanakabiliwa na mzigo mzito wa madeni.

Ghana alikoanzia ziara, ni nchi inayokabiliwa na matatizo makubwa ya kifedha na kwenda kwake nchini humo kumetajwa kuwa ni 'ziara muhimu' itakayoinua mahusiano baina ya nchi hizo mbili.

Profesa Godfred Alufar, wa Chuo Kikuu cha Ghana, alikaririwa akieleza kuwa uhusiano unaojengwa na Marekani katikati ya mgogoro wa madeni ni mzuri.

Kinachoisibu Ghana ndicho kinachoisumbua Zambia kwani taifa hilo lenye utajiri mkubwa wa madini ya shaba, linakabiliwa na mgogoro mkubwa wa madeni kutoka China.

Iko katika majadiliano na China; wakati huo huo imeomba msaada wa kifedha kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF).

Wadadisi wa mambo wameeleza kuwa matatizo hayo ya kifedha ni moja ya ajenda za Marekani ambayo inatazamiwa kuja na njia bora za Jumuiya ya Kimataifa kushughulikia madeni hayo.

**UHUSIANO NA MAREKANI**

Taarifa zinaonyesha kwamba wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu iliyoongozwa na hayati Benjamin Mkapa, Rais wa 42 wa Marekani, Bill Clinton, alitembelea Tanzania.

Wakati wa Awamu ya Nne ya Dk. Jakaya Kikwete, Marais wawili wa Marekani waliitembelea Tanzania.

Alianza George Bush, Februari, 2008 na kisha Barack Obama, Julai, 2013.

Hali hii ilidhihirisha uhusiano wa kidiplomasia uliokuwapo kati ya Tanzania na Marekani. Hata baada ya kustaafu, Bush alizuru tena Tanzania Desemba, 2011.

Taarifa zaidi zinaonyesha kwamba wakati wa Mwalimu Julius Nyerere, Baba wa Taifa alitembelea nchi ya Marekani na kukutana na rafiki yake, Rais wa 35 wa nchi hiyo, John Kennedy, White House, Julai 15, 1963 na alipokea mawaziri wawili wa Mambo ya Nje, ambao ni Henry Kissinger, ambaye alizuru Tanzania mara tatu mwaka 1976.

# AMALA
# a pekee
# lomasia




**Makamu wa Rais wa Marekani Kamala Harris (kushoto) na mwenyeji wake Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan**

Mwingine ni Cyrus Vance, ambaye alitembelea Tanzania Aprili, 1978. Ziara yake ilifuatiwa na ile ya Madeleine Albright, mwaka 1996.

Mawaziri wengine wa Mambo ya Nje wa Marekani waliozuru Tanzania ni Condoleezza Rice, aliyekuja na Bush mwaka 2008 na Hillary Clinton, mwaka 2011.

Kwa muktadha huo, ujio wa Kamala ni kipimo kuwa uhusiano wa Tanzania na Marekani umerejea kwenye hali yake ya kawaida.

Unaweza kujiuliza ni kwa nini? Kipindi cha Hayati Dk. John Magufuli, uhusiano kati yetu na Taifa hilo lenye nguvu duniani, ulighubikwa na sintofahamu kiasi cha kumpiga marufuku ya kukanyaga Marekani aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda.

Marekani pia ilikata misaada kutoka mfuko wa changamoto za malengo ya milenia.

**MILANGO ALIYOIFUNGUA KAMALA**

Katika Ikulu ya Dar es Salaam, Tanzania na Marekani zimesaini hati za ushirikiano zimesainiwa ikiwemo hati ya ushirikiano katika bandari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) na biashara.

Rais Samia amemhakikishia Mama Kamala kwamba makubaliano hayo yatatekelezwa na kuheshimiwa; na kwamba ziara hiyo itakuwa ni fursa na jukwaa la kutafuta maeneo mapya ya kuwekeza.

Rais Samia amekaribisha ushirikiano na Marekani katika maeneo ya uvuvi hasa katika bahari kuu, uvuvi wa samaki, uchimbaji wa chumvi, utafiti wa mafuta na gesi, utalii na usafirishaji wa baharini.

> **Kwa muktadha huo, ujio wa Kamala ni kipimo kuwa uhusiano wa Tanzania na Marekani umerejea kwenye hali yake ya kawaida...**

Kuhusu viza, Dk. Samia ameomba Marekani kufanya mapitio ya mkataba wake ili kuwezesha raia wa nchi hizo mbili kunufaika na viza ya muda mrefu.

Kwenye mkataba unaozipa fursa nchi za Afrika kuuza bidhaa katika soko la Marekani bila kutozwa kodi (AGOA), ameomba kwamba upitiwe upya kwa kuwa umekaribia kufikia mwisho. Nia yake ni kutaka uongozwe miaka mitano zaidi, ili umalizike mwaka 2030 badala ya 2025.

Kwenye afya, takwimu zinaonyesha kwamba kwa miongo sita, Tanzania imenufaika na misaada kutoka Marekani iliyogusa sekta kama vile afya, elimu, maji, usafi wa mazingira, kilimo, usalama wa chakula, maliasili, miundombinu, demokrasia, haki za binadamu na utawala bora.

Kwa upande wa Kamala, anasema Marekani itashirikiana na Tanzania katika maendeleo ya teknolojia ya intaneti yenye kasi ya 5G.

**BAJETI YA MAREKANI 2023/24**

Wakati Dk. Samia na Makamu wa Marekani wakiteta Dar es Salaam, Rais Joe Biden, alitoa tangazo la kuongeza bajeti ya kuimarisha demokrasia na utawala bora.

Ijumaa iliyopita, Sauti ya Amerika (VOA), iliripoti kwamba kwenye mkutano wake wa pili kuhusu demokrasia, Rais Biden aliahidi kwamba nchi yake inatenga Dola milioni 690 mwaka ujao wa fedha kuimarisha harakati za demokrasia ulimwenguni.

Katika hilo, White House imeeleza kuwa Marekani inataka teknolojia isaidie kuimarisha demokrasia.

Tayari mawaziri wakuu wa nchi nane za Ulaya wamesaini barua na kuiwasilisha kwa wakurugenzi watendaji wa kampuni kubwa za mitandao ya kijamii, wakiwataka kuchukua hatua madhubuti kwa kuzuia usambazaji wa habari za uongo kwenye mitandao yao.

Barua hiyo imesainiwa na viongozi wa Ukraine, Moldova, Poland, Jamhuri ya Czech, Estonia, Latvia, Lithuania na Slovakia.

Wakati Rais Biden akiweka msimamo huo, Ikulu jijini Dar es Salaam, Kamala aliahidi kutoa Dola milioni 16.4 kugharimia programu zinazohusu demokrasia, haki na utawala nchini.

Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), limeichagua Tanzania kama nchi itakayopokea usaidizi katika kukuza ushiriki wa wanawake na wasichana katika uongozi wa kiraia na kisiasa, hivyo kutoa takribani Dola milioni moja za nchi hiyo kugharimia programu hizo kuanzia mwaka huu.

**RAIS SAMIA**

Moyo wa maridhiano, usawa wa kijinsia, haki na uhimilivu wa kisiasa, ni maeneo yanayomtambulisha Rais Samia kwenye anga la kimataifa, kiasi cha kuaminiwa siyo tu na Afrika, bali na mataifa yenye nguvu kubwa kisiasa na kiuchumi kama Marekani.

**MAREKANI**

Marekani inatajwa kuwa ndiyo nchi maarufu zaidi duniani. Ni maarufu kwa uvumbuzi wa teknolojia, michezo na ina alama kubwa juu ya utamaduni wa kimataifa kutokana na filamu maarufu, maonyesho ya televisheni na muziki.

Taifa lenye majimbo (nchi) 50, linalojumuisha sehemu ya kati ya Amerika ya Kaskazini.

Marekani imepakana na Bahari ya Atlantiki upande wa mashariki na Bahari ya Pasifiki upande wa magharibi. Alaska, Jimbo kubwa zaidi la Marekani, linachukua peninsula kubwa kaskazini magharibi mwa Amerika Kaskazini. Jimbo la Hawaii la Marekani, ni kundi la visiwa linalopatikana katikati mwa Bahari ya Pasifiki, kusini-magharibi.


Marekani inapakana na Canada upande wa kaskazini na mpaka wake wa kusini una urefu wa kilomita 3,155 hadi Mexico.

Marekani pia inashirikiana mipaka ya baharini na Bahamas, Cuba, na Urusi.

Ikiwa na eneo la kilomita za mraba 9,833,516, Marekani ni nchi ya tatu kwa ukubwa duniani, ikiwa na ukubwa wa zaidi ya mara mbili ya Umoja wa Ulaya au karibu nusu ya ukubwa wa Urusi.

Marekani ina idadi ya watu milioni 330, (mwaka 2021); ni nchi yenye watu wengi zaidi katika bara zote za Amerika.

Mji mkuu wake ni Washington D.C, Jiji kubwa zaidi ni New York na asilimia 80 ya watu wake wanazungumza Kiingereza.



**Rais Mstaafu wa Marekani George Bush wa Marekani akiwa na mwenyeji wake Rais Mstaafu Rais Jakaka Kikwete akizungumza na waandishi wa habari alipofanya ziara ya kikazi nchini Tanzania wakatika akiwa madarakani.**

Siasa

# M'kiti wa Serikali ya Mtaa anayefanya maajabu ya uongozi licha ya ulemavu

**Na Claudia Kayombo**

NI mwanamke mwenye haiba ya kujiamini, mpole, msikivu na mwenye huruma. Ni mwepesi wa kusikiliza shida ya mtu na kuitafutia ufumbuzi wa haraka na wenye tija.

Wenye shida wanapotoka mbele yake, huonesha furaha, kwa kuwa wanakuwa wametatuliwa shida zao.

Ana lugha ya upendo na kujali dhidi ya watu wanaomjongelea, anaonesha amani anapomaliza shida ya mtu ambayo alikuwa na jukumu la kuitatua. Unapomuona kwa mara ya kwanz, huwezi kubaini iwapo ni mlemavu wa mguu mmoja kwa kuwa hali hiyo haimzuii uthubutu wa kufanya mambo mengi yenye tija katika eneo lake, pengine kuliko hata aliye timamu wa viungo.

Huyu ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Zavara, Chanika jijini Dar es Salaam, Chiku Mwalutambi (CCM).

Nilibaini hayo muda niliokuwa katika viunga vya ofisi yake kwa muda nikisuburi zamu yangu ya kumUona.

Awali, alidhani nami ni mmoja wa wananchi wake tuliokuwa tukisuburi kukutana naye kwa ajili ya kupatiwa huduma mbalimbali za kiofisi.

La hasha, nilikuwa mgeni kutoka mbali na eneo hilo ambaye hakuwahi kuniona, wala kusikia habari zangu, hata hivyo, aliponiona kwa mara ya kwanza kabla ya kujitambulisha, alinionesha tabasamu.

Mwanamke huyu ambaye ameshawahi kwenda Beijing, China mara mbili kudai haki za walemavu wanawake nchini, ni mwerevu labda ni kutokana na bahati hiyo ya kusafiri nchi mbalimbali duniani ambako amekutana na watu wa aina tofauti.


"Mwaka 1992, nilikuwa Mkuu wa Idara ya Jinsia upande wa Walemavu Tanzania ndani ya Chawata (Chama cha Walemavu Tanzania).

"Nilikwenda Beijing Septemba, 1995 na mwaka 2000, kabla ya hapo niliwahi kwenda Accra Ghana, Sudan, Sudan Kusini, Zambia, Zimbabwe, Afrika Kusini, Malawi, Uganda, Kenya na Ethiopia, kote huko nilikwenda kudai haki za walemavu, anasema na kuongeza:

"Unakwenda mahali, unawakuta wazungu watupu, mweusi peke yako, nao pia wanataka kukusikia unasemaje kutetea walemavu na wanawake wan chi yako."

Anasema: "Nikafanya kazi ya kuelimisha kinamama na watu wa kawaida, hivyo tulikuwa tunazungumza na waziri husika, tulikuwa tunafanya makongamano serikalini, bungeni na maeneo mengine.

Anaongeza: "Ninachofurahi mimi kwamba, elimu kuhusu haki za walemavu nchini imefahamika, mwaka 2000 nilikwenda Umoja wa Mataifa kutoa matokeo baada ya Mkutano wa Beijing."



Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Zavara, Chanika jijini Dar es Salaam, Chiku Mwalutambi (CCM).

> **Hadi Novemba, mwaka jana, jumla ya zabuni 28 zenye thamani ya Sh. bilioi 10.318 za awamu ya kwanza, zilikamilika na walianza kazi...**

Chiku anasema katika ziara hizo alizofanya mwaka 1995 na 2000, kikubwa alikuwa akiwasilisha mafanikio ya taifa kuhusu haki za walemavu.

Chiku anasema hii ni awamu ya pili anaongoza mtaa huo unaounda Kata ya Buyuni Jimbo la Ukonga, Manispa ya Ilala, Dar es Salaam na kwamba anajisikia amani kuwahudumia wananchi katika nafasi hiyo.

"Kitu ambacho nimejifunza, ukiwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, kuna wakati unakuwa hakimu pale unapoamua ugomvi baina ya wanandoa au wananchi wa kada nyingine, wakati unakuwa askari polisi unapotoa amri mtuhumiwa akamatwe, wakati mwingine unakuwa mwalimu unapowaelimisha wananchi wafuate njia fulani nzuri na waachane na njia isiyofaa na pia unakuwa imamu au katekista ambapo unalazimika kuwahubiria Neno la Mungu," anasema na kuongeza:

"Binafsi, naipenda hii kazi na wala siijutii, licha ya kuwa hapo awali niliwahi kugombea ubunge wa makundi maalum walemavu, lakini sikufanikiwa.

Akizungumzia historia yake hadi alipofikia anasema: "Nilianza kuwa Katibu wa Chawata Mkoa wa Tabora mwaka 1982.

"Nimepita Tanzania nzima kuanzia mwaka 1996 hadi 2000 nikitoa elimu ya umuhimu wa mikopo kwa watu wenye ulemavu na kuwapatia mikopo hiyo."

"Mwaka 2005, tulianza kutoa mikopo kwa watu wasio na ulemavu.

Akizungumzia namna alivyoingia katika

Inaendelea Uk.15

Siasa

# M'kiti wa Serikali ya Mtaa anayefanya maajabu ya uongozi licha ya ulemavu

Inatoka Uk.14

siasa, Chiku anasema: "Nilikuwa Mjumbe wa Shina namba 6, kuanzia mwaka 2012 hadi 2014.

"Baada ya kukata mitaa mwaka 2014, baadhi ya wananchi wenzangu wakanifuata kuniomba niingie serikali ya mtaa nigombee Uenyekiti.

"Niligombea na wanaume saba, nilikuwa mwanamke pekee na niliwashinda. Wakati wa kampeni, wapinzani walikuwa wanatumia ulemavu wangu kunidhalilisha."

"Mgombea wa CUF akawa anapiga kelele kuwa wasinichague mtaa utakuwa ombaomba, akasema asili ya walemavu ni kuomba Mnazi Mmoja," anasema Chiku.

Anabainisha kuwa, Desemba 14, 2014, ndipo alipochaguliwa kwa mara ya kwanza na aliapishwa Januari 8, mwaka 2015.

"Nilipewa rasilimali watu na ardhi. Mtangulizi wangu aliniambia huku kuna maeneo saba ya kujenga huduma za jamii.

"Baada ya kuingia madarakani, tulikubaliana na wananchi tuchangie Sh. 5,000 kwa ajili ya kujenga shule, nimesimamia wazo hilo, tumejenga shule ya msingi na sekondari katika eneo la ekari 12." Anasema Chiku kwa kujiamini.

"Nimepata vyumba vinane vya Uviko 19 ambapo nimepewa milioni 160," anafafanua.

Aidha, anasema amejenga pia ofisi ya serikali ya mtaa na ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), katika yale maeneo saba aliyokabidhiwa na mtangulizi wake.

"Nimeanza kujenga kituo cha polisi, asilimia 70 ya wananchi wangu tayari wana umeme wa Rea, maji ya Dawasa yapo na pia kuna visima 40 vifupi vimejengwa na wafadhili.

"Ninavyo visima virefu vinne, nina shule ya msingi na sekondari, eneo tunalotarajia kujenga hospitali kuna kisima, kingine kimejengwa katika maeneo ya wananchi kuwasogezea huduma.

"Maji ya Dawasa ninayo, zimebaki nyumba tano tu kukamilisha, hivyo naweza kusema katika eneo langu, hakuna shida ya maji, watu wanachagua maji wanayotaka kutumia.

"Barabara mbili na makaravati kutoka Kwa Sadala hadi shule ya msingi na sekondari zimejengwa kwa msaada wa Tarura.

"Kutoka kwa Zoo kuingia ndani kutenganisha Mtaa wa Zavara na Buyuni, kumejengwa makaravati.

"Mazingira mazuri ya kujifunzia kwa shule ya msingi na sekondari yanachochea ufaulu.

"Zavara katika kata yetu, ni ya kwanza katika ufaulu ni ya 16 kiwilaya.

"Nimezuia vifo vya watoto vilivyokuwa vinatokana na kugongwa na magari au kuzolewa na maji wakati wa masika kwa kufuata elimu mbali na maeneo yao.

"Usimamizi mzuri wa Mkuu wa Shule ya Sekondari, Magnus Kayombo, wazazi na uongozi wa mtaa, umesaidia ufaulu huo.

"Hata sekondari ya kata, wanafanya vizuri, hakuna daraja la mwisho, daraja la Kwanza na Pili ni wengi sana, la tatu na la nne ni wachache, hakuna daraja sifuri.

> **Baada ya kuingia madarakani, tulikubaliana na wananchi tuchangie Sh. 5,000 kwa ajili ya kujenga shule, nimesimamia wazo hilo, tumejenga shule ya msingi na sekondari katika eneo la ekari 12...**

Kuhusu ulinzi na usalama wa mtaa huo, anasema vikundi vya ulinzi shirikishi vipo tisa na Amepata cheti cha kufanya vizuri kutoka Jeshi la Polisi wilaya kiposi Chanika cha kutambua kazi yake.

"Wakati naanza, haya hayakuwapo. Nipo njiani kuanza kujenga zahanati ya mtaa wetu, sasa huduma za afya wananchi wanafuata Buyuni, Nguvukazi, Pugu na Kisarawe.

"Tunajipanga kujenga soko, tuna changamoto ya ukosefu wa vyumba vya madarasa ya kutosha ya sekondari, jengo la utawala na maabara, naomba serikali inisaidie."

Hata hivyo, anasema serikali iliniahidi kujenga majengo matatu ya ghorofa tatu tatu kwa ajili ya kidato cha tano na sita.

"Kwa kujenga msingi, nimeomba Memkwa na shule maalum kwa walemavu, pia darasa la elimu ya watu wazima.

"Tarura wameahidi kutujengea vivuko vitano wanasubiri bajeti, wenyewe kwa harambee, baadhi tumetumia fedha kidogo kwa ajili ya kununua misumari."

Chiku anasema anafurahi ametekeleza Ilani ya CCM kwa asilimia 99.9.

Akizungumzia changamoto alizokutana nazo akiwa Mwenyekiti, Chiku anasema alikaa gerezani kwa wiki mbili kwa agizo la aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, baada ya wapinzani wake kisiasa kumfikishia tuhuma za kuuza ardhi ambapo awali aliumia, lakini alijikuta ujasiri unaongezeka kila siku zilivyosonga.

"Makonda nimemsamehe duniani na ahera," anasema Chiku.

Kuhusu elimu yake, anasema ni ya kidato cha nne ambayo zamani ilikuwa na thamani kubwa tofauti na sasa.

Akizungumzia hali ya watu wenye ulemavu nchini kwa sasa Chiku anasema: "Nampongeza Waziri Jenista kwa kazi nzuri aliyoifanya alipokuwa katika wizara ile, alikuwa anawazungumzia haki zao kana kwamba na yeye ni mwenye ulemavu."

"Jambo linalonifurahisha ni kuona shule zangu zinafanya vizuri, imewafanya watu kunisikiliza na kunipa msaada," anasema.

## MAKALA BIASHARA



## DONDOO MUHIMU ZA KUFANIKIWA

NDOTO za kila mtu, ni kufanikiwa katika maisha yake.
Kila uchao, binadamu hupambana ili kuifikia ndoto hiyo. Zifuatazo ni dondoo muhimu za dhana ya kufanikiwa:-

1. Kuwa na wazo na hakikisha limeandikwa. Baada ya kuwa na wazo na kuliandika, hatua inayofuata kuhusu wazo lako ni kuanza utafiti juu ya wazo hilo ili kujua kama ni la maana au hutakiwi kuendelea nalo.

2. Tenga muda ambao utafanyia kazi wazo lako. Usipoweka muda, hutaweza kujipima.

3. Jifunze kwa waliotangulia kisha ufanye kwa ubora. Kama kuna habari za wazo lako, nenda usome, kama kuna waliokwisha kufanya, wasikilize. Usikimbilie tu kuanza, kama kuna jinsi ya kupata taarifa, basi zitumie kwanza.

4. Lipange wazo lako kwa kuligawa kwenye malengo madogo madogo yenye sifa kubwa tano.
   Uwe na malengo maalum
   Weka wazo kwenye malengo
   yanayopimika
   Hakikisha wazo lako linatekelezeka.
   Hakikisha ni wazo la maana.
   Tenga muda maalum kwa wazo kutekelezwa.

5. Hakikisha unatengeneza au kujiunga na mtandao wa watu wenye maono kama yako. Ni rahisi kupata mafanikio ukiwa na watu wenye malengo na maono kama wewe. Mafanikio yako yanategemea sana na watu waliokuzunguka.

6. Anza sasa kulitekeleza. Usingoje kesho wala usiahirishe.
7. Kuwa mbunifu, usiishi kwa mazoea, fikiria nje ya kawaida.

8. Lazima kupata watu utakaoshirikiana nao (In a win – win situation) kukufikisha kwenye lengo. Hata kama wazo ni dogo, utahitaji watu kukusaidia. Ni muhimu kuwa makini kuhakikisha vitu vyote muhimu vimezingatiwa wakati wa kufanya uamuzi huo sababu aina ya watu utakaokuwa nao, ndiyo aina ya mafanikio ya wazo lako.
   Kama unataka kufanikiwa, lazima uwe na wazo la kukufikisha kwenye mafanikio unayoyahitaji.
   Bila kuwa na wazo lolote ila unawaza kupata kazi na mshahara pekee, sahau kabisa neno au dhana ya mafanikio maishani mwako.
   Hamasa ya somo hili ni kukupa azma ya kuandaa mafanikaio yako mwenyewe.
   Hatukwambii kuwa itakuwa rahisi, ila lazima uwe na wazo na ujipange kwa mujibu wa kanuni za mafanikio ndipo uingie kwenye safari ya wanaohitaji kufanikiwa.

## Utalii



# Maajabu, sifa na tabia ya ndege Mbuni mkubwa

**MBUNI ni ndege zaidi kuliko wote duniani.**

HATA hivyo, licha ya ukubwa aliokuwa nao, hana uwezo wa kupaa kama walivyo ndege wengine. Ukimshangaa mbuni asiyepaa, utamstaajabu ngwini, samaki asiyepaa mwenye uwezo wa kuogelea. Ana matumbo matatu ya kuhifadhia chakula. Ana uwezo wa kukimbia kwa kasi ya kilomita 70 kwa saa.

**Mbuni ana vidole viwili kwenye mguu wake mmoja.**

Kawaida, ukimkuta mbuni ndani ya Hifadhi ya Taifa yoyote hapa nchini kama vile Ngorongoro, Serengeti, Mikumi na nyingine, mbuni anavyovimba akiwa amejichanganya na pundamilia na nyumbu wakitafuta malisho, unaweza kujisahaulisha kuwa huyu ni ndege na huenda ukadhani ni jamii ya wanyama wengine kulingana na ukubwa wake. Watu wengi wamekuwa wakimuona mbuni kama ndege wa kipekee na wa tofauti, basi kama unaisoma hii makala utajua tofauti. Pia tofauti kati ya mbuni na ndege wengine kupitia sifa zake 10.

**Sifa 10 za mbuni**

**1. Muonekano**

Mbuni ndiyo ndege mrefu, mkubwa na mzito zaidi duniani, ana wastani wa kilo 50 kama mbuzi, lakini pia ana uzito sawa na kuku 20. Hii inaweza kuwa ndiyo sababu kuu inayomfanya ashindwe kupaa.

**2. Mfumo wa mmeng'enyo wa chakula**

Mbuni ana matumbo matatu na ni ndege pekee ambaye haja zake ndogo na kubwa, hutoka tofauti, yaani hazijichanganyi.

**3. Mbio na kasi**

Mbuni ana uwezo wa kukimbia kwa kasi ya kilomita 70 kwa saa, kasi kubwa kuliko ndege yoyote yule. Hatua yake moja ni sawa na hatua tano za binadamu.

**4. Vidole**

Tofauti na ndege wengine wenye vidole vinne ambapo vitatu huangalia mbele na kimoja nyuma, mbuni ana vidole viwili kwenye mguu wake mmoja, vyote vinaangalia mbele.

**5. Kujihami**

Kwenye hatari, silaha kubwa ya mbuni huwa ni mateke yake, hurusha mateke ya mbele yenye uwezo wa kuua wanyama wakali kama fisi, chui hata simba. Teke moja la samba, lina uwezo wa kuua adui.

**6. Tabia za misimu**

Katika msimu wa masika, mbuni hukaa peke yake au na mpenzi wake na katika msimu wa kiangazi, mbuni hukaa katika makundi ya mbuni wengi hadi 50 na hupenda kujichanganya na makundi ya swala na pundamilia.

**7. Mapenzi yao ni ya kipekee**

Maajabu, mbuni ana utaratibu wa kipekee sana. Kwanza mbuni dume hupiga mabawa yake kama anataka kupaa ikiwa ni ishara kwamba anatafuta mwenza.

Akishapata mwenza, wanaanza kutafuta malisho na anahakikisha anampeleka sehemu ambapo hakuna wanyama wengine na wanaendelea kutafuta malisho hapo huku wakizoeana tabia.

Baadaye, mbuni dume huanza tena kupiga mabawa kwa nguvu zaidi na kuzunguka akiwa ameyashusha huku akidonoa udongo, ambapo jike la mbuni likishaona hizo ishara, basi huchuchumaa na kumruhusu.

**8. Yai la mbuni**

Mbuni zaidi ya mmoja, hutaga mayai yao kwenye tundu moja na kila mbuni ana uwezo wa kutofautisha mayai yake na ya mbuni wengine.

Yai la mbuni lina uzito wa zaidi ya kilo moja na ukubwa sawa na nazi. Yai moja la mbuni ni sawa na mayai yasiyopungua 20 ya kuku.



> Watu wengi wamekuwa wakimuona mbuni kama ndege wa kipekee na wa tofauti, basi kama unaisoma hii makala utajua tofauti...

**9. Jike na dume wote huatamia mayai**


Jike la mbuni ana rangi ya kijivu na huatamia mayai mchana kwa sababu rangi yake hufanana na mchanga, hivyo ni ngumu kuonekana na adui, dume la mbuni lina rangi nyeusi hutamia mayai usiku kwa sababu ni ngumu kuonekana gizani. Mayai ya mbuni huchukua siku 35 mpaka 45 kutotolewa.

**10.Macho makubwa**

Jicho la mbuni linalingana na yai la kuku, jicho la mbuni ni kubwa kuliko ubongo wake. Hivyo ana uwezo mkubwa sana wa kuona mbali na kwenye giza.

Mbuni ni ndege asiyeonekana kirahisi kwa sababu idadi yao imepungua sana hivyo kuwaona ni mpaka mbugani, kwenye hifadhi au kwenye mashamba ya watu binafsi wanapofugwa.

**HABARI**KUTOKA ZANZIBAR



# Mfumo wa taarifa utapunguza migogoro ya ardhi - Waziri

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, Rahma Kassim Ali, amesema kuwepo kwa mfumo wa taarifa za usimamizi na usajili wa ardhi, utasaidia kwa kiasi kupunguza migogoro ya ardhi iliyokuwepo visiwani humu.

Aliyasema hayo baada ya kushuhudia utiaji saini wa hati ya makubaliano kati ya wizara hiyo na Shirika la Kitaifa la Kijografia na Misitu ya Ufaransa (IGN FI) kuhusu mfumo huo uliofanyika katika ofisi za wizara hiyo Maisara.

Alisema wamekuwa wakishuhudia migogoro mingi ya ardhi ambayo kila siku na huchukua muda mrefu, na mfumo huo sasa utasaidia kupunguza migogoro.

Hivyo alisema kutokana na mfumo huo, mmiliki atakuwa akijulikana kwenye mfumo na kuwa ndiye mhusika wa eneo la ardhi analolimiliki.

"Sasa hivi taarifa nyingi zimekaa na inachukua muda mrefu na kupotea, lakini mfumo kama mfumo, inakuwa siyo rahisi kupoteza taarifa zake," alisema.

Alisema hivi sasa wanataka kwenda kwa haraka ili kuendana na agizo la serikali la kuitambua ardhi yote ambayo ni katika shehiya zote 388 za Zanzibar.

Aliongeza kuwa anaamini wakishafanya utambuzi wa ardhi na taarifa kuingia kwenye mfumo, asilimia 95 ya migogoro ya ardhi itakuwa haipo na itakayobakia ni ile ya kawaida, lakini lile tatizo kubwa linaloikumba wizara, litaondoka.

Alisemsa hiyo itakuwa ni manufaa makubwa ambayo Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinyi, itakuwa imepiga hatua kubwa.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Mngereza Mzee Miraji, alisema mfumo huo utakapoanza kazi, utakuwa na faida kuu sita ikiwemo ya kuongeza usalama wa umiliki wa ardhi kwa wawekezaji na wananchi, kupunguza urasimu na kutoa huduma rahisi ya kuaminika na salama kwa mteja kwani wananchi na wawekezaji wamekuwa wakitoa malalamiko katika jambo hilo.

Nyingine ni kupunguza muda wa kukagua, kusahihisha na kubadilisha ama kuhamisha umiliki wa ardhi kwa wananchi wawekezaji na miradi yote inayofanyika Zanzibar, kupunguza uvamizi wa ardhi, misitu, hifadhi za barabara na sehemu za wazi, uhifadhi wa ardhi na maliasili na kupunguza rushwa na viashiria vyote vya rushwa hasa wa ufuatiliaji, usajili na uhamisho wa hatimiliki.

Dk Miraji alisema utiaji saini huo ni mwanzo mpya ya kimapinduzi katika sekta ya ardhi nchini ambayo ndiyo lengo la Rais wa Zanzibar ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Mwinyi kuondoa urasimu na migogoro ya ardhi Zanzibar.

Mapema, Mrajis wa Ardhi, Dk. Abdul-Nasser Hikmany, alisema mfumo huo utasaidia kiutendaji pamoja na kutoa huduma bora kwa jamii.

> **Sasa hivi taarifa nyingi zimekaa na inachukua muda mrefu na kupotea, lakini mfumo kama mfumo, inakuwa siyo rahisi kupoteza taarifa zake...**

Alisema ni malengo yao kuwa taarifa zote zitakazohusu ardhi, zitaingizwa katika mfumo huo ikiwemo utambuzi, mipango miji, usajili na mambo mengine.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kitaifa la Kijiografia na Misitu la Ufaransa (IGN FI), Christopher Dekeyne, aliipongeza serikali kufanya kazi pamoja na shirika hilo katika utekelezaji wa mfumo ambao utasaidia kubadili usimamizi wa ardhi Zanzibar.

Alisema wamefarajika kuona umuhimu uliowekwa na serikali kupitia Wizara na watu wa Zanzibar katika kuutaka mfumo huo na wana uzoefu mkubwa katika mabara mengi hasa Afrika na wapo tayari kuonesha uwezo wao na kuhakikisha wanafanikiwa na mradi huo unaleta manufaa kwa Zanzibar.

## ZRA yakusanya bilioni 449/- kwa miezi tisa

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

MAMLAKA ya Mapato Zanzibar (ZRA), imekusanya jumla ya Sh. bilioni 449.283 sawa na asilimia 97.56 ya makusanyo ya kodi ya kiasi cha Sh. bilioni 460.499 bilioni katika kipindi cha miezi tisa ya mwaka wa fedha 2022/2023. (Julai – Machi).

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari ofisini kwake Mazizini visiwani humu, Kamishna Mkuu wa ZRA, Yussuph Juma Mwenda, alisema makusanyo halisi ya miezi tisa hiyo kwa mwaka 2022/2023 yameongezeka kwa asilimia 63.50 ukilinganisha na makusanyo halisi ya kodi ya miezi tisa kwa mwaka uliopita wa 2021/2022 ambayo yalikuwa Sh. bilioni 274.799.

Alisema kwa kipindi cha miezi mitatu Julai hadi Septemba, makusanyo halisi yalikuwa Sh. bilioni 82.951 makisio ni Sh. bilioni 135.125 ambapo makusanyo halisi yalikuwa ni bilioni 131.793 sawa na ufanisi wa asilimia 97.53 na ongezeko la makusanyo halisi ni Sh. bilioni 48.842 sawa na ukuaji wa asilimia 58.90.

Kwa robo ya pili kuanzia Oktoba hadi Desemba, mwaka 2022 alisema makusanyo halisi yalikuwa ni shilingi bilioni 87.217, makisio 154.923 ambapo makusanyo halisi yalikuwa ni 154.299 sawa na ufanisi wa asilimia 99.60 na ongezeko la makusanyo halisi ni Sh. bilioni 67.082 sawa na ukuaji wa asilimia 76.92.

Kamishna Mkuu Mwenda alibainisha kuwa kwa robo ya tatu ya mwezi Januari hadi Machi, makusanyo halisi ni Sh. bilioni 104.630, makisio ni Sh. bilioni 170.451 ambapo makusanyo halisi ni Sh. bilioni 163.189 ufanisi wa asilimia 95.74 ongezeko la makusanyo halisi ya Sh. bilioni 58.559 sawa na ukuaji wa asilimia 55.97.

Aliongeza kuwa mafanikio ya ufanisi wa asilimia 97.56 na ongezeko la la kodi la kiasi cha Sh. bilioni 174.484 katika kipindi hicho cha miezi tisa ya mwaka 2022/2023, yamechangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo kuimarika kwa huduma kwa walipa kodi.

Alisema ZRA imeendelea kuimarisha huduma za kikodi kupitia ofisi zake za Mikoa ya kodi ya Unguja na Pemba na kiwango cha utoaji wa elimu kupitia semina, mikutano na walipa kodi, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ikiwemo ZRA Oline TV, vimeongeza ulipaji wa kodi wa hiari.

Sababu nyingine alisema ni matumizi ya mfumo katika ukusanyaji wa mapato (VFMS) na upatikanaji wa wakati wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ndani ya mamlaka hiyo, imechangia ukuaji mzuri wa mapato katika kipindi hicho.

Kamishana Mwenda alisema mambo mengine ni weledi na uadilifu kwa wafanyakazi na uwajibikaji wa hiari wa walipa kodi ambapo kutowajibika kwa baadhi ya walipa kwa hiari ikiwemo kutotoa risiti za kielektroniki, kumechangia kutofikia ufanisi wa asilimia 100.

Hata hivyo, alisema katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya kodi katika robo ya nne ya mwaka wa fedha 2022/2023, ZRA itaendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa kodi ikiwemo kuanza kwa mfumo mpya wa usimamizi wa ukusanyaji wa kodi wa ZIDRAS ambao utaunganishwa na mifumo mengine ikiwemo mfumo wa Immigration na Tanciss.




**WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, Rahma Kassim Ali, akishuhudia utiaji saini wa hati ya makubaliano kati ya wizara hiyo na Shirika la Kitaifa la Kijiografia na Misitu ya Ufaransa (IGN FI) kuhusu mfumo wa taarifa za usimamizi na usajili wa ardhi uliofanyika katika ofisi za wizara hiyo Maisara. Katibu Mkuu wa Wizara, Dk. Mngereza Mzee Miraji, alitia saini kwas niaba ya wizara yake na wa IGN FI,Mkurugenzi Mkuu Christoph Dekeyne, alifanya hivyo kwa niaba ya shirika lake. (Picha: Mpigapicha Wetu)**


Alisema Mamlaka hiyo itaendelea kuwataka wananchi kuendelea kudai risiti za kielektroniki kila wanapofanya manunuzi na kuwahimiza wafanyabiashara kutoa risiti wanapofanya mauzo sambamba na kuendelea kuchukua hatua za kisheria kwa wafanyabiashara wakubwa ambao hawajaunganisha mifumo yao na mfumo wa VFMS.

Sambamba na hayo, alisema ZRA itaendelea kutoa elimu na huduma ya kodi na kujenga weledi na uaminifu wa watumishi wake.

Aidha, alimpongeza Rais wa Zanzibar ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi na viongozi wengine wa serikali kwa uhamasishaji na miongozo yao inayorahisisha ulipaji kodi wa hiari Zanzibar na watumishi wanaotimiza wajibu wao kuhakikisha ulipaji kodi wa hiari unaimarika.

Kadhalika, aliwashukuru walipakodi wote kwa kulipa kodi kwa hiari na kuwataka kuendelea kushirikiana na mamlaka hiyo ili kuiwezesha serikali kupata mapato yake kwa ajili ya kupeleka huduma za kimaendeleo kwa wananchi ikiwemo elimu, afya, maji safi na salama na miundombinu.

**MWENYEZI MUNGU TUNAKUOMBA DUA UMPE MAISHA MAREFU,AFYA NJEMA, NGUVU ZAIDI NA MAFANIKIO ,RAIS WETU MPENDWA DK. SAMIA SULUHU HASSAN**



# Kenya kuzindua satelaiti ya uchunguzi wa dunia

**NAIROBI, Kenya**

KENYA inajiandaa kurusha satelaiti yake ya kwanza kabisa ya uchunguzi wa dunia katika kile kinachoelezwa kuwa mafanikio ya kihistoria katika juhudi za uchunguzi wa anga la juu nchini humo.

Nation-1 au Taifa-1 kwa Kiswahili, imeratibiwa kurushwa wiki ijayo kwa roketi ya SpaceX Falcon 9 kutoka kituo cha anga cha Vandenberg huko California.

Satelaiti hiyo imeundwa ili kutoa data ya uchunguzi wa ardhi kwa ajili ya matumizi ya kilimo, usalama wa chakula na usimamizi wa mazingira, Wizara ya Ulinzi na Shirika la Anga la Kenya zilisema katika taarifa ya pamoja. "Iliundwa kikamilifu na kuendelezwa" na wahandisi wa Kenya kwa ushirikiano na mtengenezaji wa anga ya Bulgaria, taarifa hiyo iliongeza.

Ujumbe kutoka Kenya unatarajiwa kusafiri hadi Marekani kwa ajili ya uzinduzi huo.

Misheni hiyo inaonekana kama hatua muhimu kwa uvumbuzi wa kisayansi wa Kenya.

Nchi hiyo inakabiliwa na ukame mbaya zaidi kuwahi kutokea katika miongo kadhaa baada ya misimu mitano ya mvua kushindwa.

Mwaka 2018, Kenya ilizindua majaribio yake ya kwanza ya satelaiti ya ano kutoka Kituo cha Kimataifa cha Anga za Juu.

**BBC**

> **Iliundwa kikamilifu na kuendelezwa" na wahandisi wa Kenya kwa ushirikiano na mtengenezaji wa anga ya Bulgaria...**



SpaceX Falcon 9

## Israel yaongeza shambulizi Damascus

**JERUSALEM, Israel**

SHAMBULIZI la anga la Israel limeulenga Mji Mkuu wa Syria, Damascus, mapema jana kulingana na ripoti ya chombo cha habari cha serikali likiwa la nne mjini humo tangu Alhamisi wiki iliyopita.

Wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyodumu kwa zaidi ya muongo mmoja nchini Syria, Israel imefanya mamia ya mashambulizi nchini humo, ikilenga vikosi vinavyoungwa mkono na Iran na wapiganaji wa Hezbollah wa Lebanon na Jeshi la Syria.

Chombo cha habari cha serikali ya Syria, SANA, kimesema kwamba mfumo wake wa ulinzi wa anga umenasa makombora kadhaa kwenye anga ya Damascus, akiashiria mashambulizi kutoka Israel.

Hata hivyo, awali chombo hicho kiliripoti sauti ya mlipuko karibu na Damascus.

Shirika la kutetea haki za binadamu la Syrian Observatory for Human Rights linalofuatilia mapigano nchini humo,limesema kwamba silaha za Israel zimekuwa zikilenga kituo cha Iran kilichoko karibu na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Damascus.

## ...EAC: Amani imeanza kurejea DRC

**NAIROBI, KENYA**

MRATIBU wa mazungumzo ya amani Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki, Rais wa zamani wa Kenya, Uhuru Kenyatta, amesema hatua imeanza kupigwa kurejesha amani na utulivu katika mikoa ya Mashariki mwa DRC.

Kenyatta, kupitia kwa taarifa yake amesema baada ya mikutano mitatu ya Marais wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu hali ya usalama Mashariki mwa DRC, hali ya utulivu inashuhudiwa jimboni Kivu Kusini, lakini pia visa vya mashambulio vimepungua huko Kivu Kaskazini ingawa bado ni ya kutia wasiwasi.

Hata hivyo, amesema juhudi za kutoa misaada ya kibinadamu kwa watu walioathiriwa na utovu wa usalama, zinaendelea vema na jeshi kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki, limeanza kuchukua miji na vijiji vilivyokuwa vinashikiliwa na makundi ya waasi.

Aidha, mratibu huyo amedokeza kuwa, mipango inaendelea ili kuandaa mkutano wa wadau wote wa mzozo huo pamoja na watalaam kutoka nje ya nchi, kutathmini namna ya kupata suluhu ya kisiasa, mazunngumzo yatakayofanyika Mashariki mwa DRC.

Kuhusu kuondoka kwa waasi wa M 23 katika maeneo wanayoshikilia, Mratibu huyo amedokeza kuwa kundi hilo litaondoka kutoka maeneo ya Sake, Mshaki, Neero na Kilolirwe kuanzia jana na hii inakuja baada ya kuwasili kwa wanajeshi wa Sudan Kusini mwishoni mwa wiki iliyopita.

Kikosi cha Kenya kipo katika eneo la Kibati, Kibumba na Rumangambo, kile cha Burundi kikiwa katika eneo la Sake, Mshaki na kinatarajiwa kwenda Kitchanga na kile cha Uganda ambacho kipo Bunagana, kinatarajiwa kudhibiti kiwanja ifikikapo Aprili 15, mwaka huu.



## DRC yaongeza muda wa utekelezaji sheria ya kijeshi

**KINSHASA, DR Congo**

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imeongeza muda wa sheria ya kijeshi kwa mara ya 45 katika mikoa ya mashariki ya Kivu Kaskazini na Ituri ambako uasi wa miongo kadhaa unaendelea.

Ongezeko hilo la siku 15, lilianza Jumapili iliyopita, kwa mujibu wa Mishapi Voice Radio.

"Kulingana na Waziri wa Sheria, Rose Mutombo, ambaye aliwasilisha muswada huo kwa Baraza la Seneti Jumamosi iliyopita, lengo ni kuruhusu jeshi la DRC kuwa na njia zote zinazohitajika ili kuendelea na operesheni za kijeshi na kukomesha kabisa ukosefu wa usalama unaoendelea katika eneo hili la mashariki mwa nchi hiyo," redio hiyo iliripoti.

Hali ya kuzingirwa, ambayo ni utawala maalum wa sheria ya kijeshi, iliamuliwa katika majimbo hayo mawili na Rais Félix Tshisekedi Mei, 2021.

Lengo lilikuwa kudhibiti ghasia za waasi waliotoroka katika majimbo hayo mawili kwa kuweka tawala za kijeshi na kuimarisha operesheni za usalama.

Uasi upya wa Vuguvugu la (M23) huko Kivu Kaskazini, umeongeza shughuli zaidi huku rasilimali zikielekezwa kukabiliana na uvamizi huo.

# Pata nakala laini ya gazeti lako la Uelekeo

Kila siku ya Jumatano uhabarike

Habari | Makala | Michezo na Burudani






## Hongera Mheshimiwa Rais

Miaka 2

ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**

Tunakutakia kila la kheri katika kazi zako za kuongoza taifa la Tanzania kuelekea kufikia mafanikio zaidi.






Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wales Karia akiwa na Katibu Mkuu wa Shirikisho hilo,Wilfred Kidao wakiwa katika moja ya vikao vya kujadili masuala ya soka. Picha na Mtandao

# Kuionea TFF ni kutegemea kuzalisha Stars ya baadae

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU ile Simba ilipopokea kichapo cha mabao 3-0 kikosi cha Raja Casablanca iliyocheza na wawakilishi hao wa Tanzania katika michuano ya Klabu Bingwa Afrika, kilijaa sura za wachezaji vijana halisi.

Picha za runinga zikimuonesha mchezaji anayetoka akiwa hana tofauti kubwa ya umri na yule anayeingia. Nguvu ile ile waliyoanza nayo ndiyo waliyomaliza nayo.

Wakati Joash Onyango akionekana kabisa kuishiwa nguvu dakika zile za 80 kuelekea 90, mshambuliaji wa Raja alikuwa kama vile ndiyo kwanza ameingia uwanjani.

Pale katikati Waarabu wale kutoka Morocco walipasambaratisha, hakuonekana Cloutus Chama wala Saido Ntibazonkiza. Kikosi kile kilijaa wachezaji walioandaliwa pale pale Morocco.

Miezi michache kabla timu yao ya taifa, ilikua imetoka kucheza mechi ya kutafuta mshindi wa tatu wa Kombe la Dunia kule Qatar 2022.

Wale walikua ni vijana wa Raja Casablanca bado wapo vijana wa Wydad Casablanca na wa timu nyingine za Ligi Kuu nchini Morocco.

Na kuna kundi la vijana wanaozaliwa na kukulia Ulaya wakiwa na hati za kusafiria za Morocco, hukua kimpira wakiwa bara jingine.

Niliitazama timu ya Vipers ya Uganda ilivyowasumbua Simba walipocheza mechi ya marudiano ya Klabu Bingwa Afrika jijini Dar es Salaam ambapo wenyeji walishinda bao 1-0.

Ile ilikuwa ni timu iliyoundwa na wachezaji wengi waliokuzwa katika mfumo wa timu za vijana, uliozoeleka nchini Uganda.

Kikosi chenye wachezaji wa kigeni wasiozidi watano uwanjani na kikawasumbua Simba, wenye uzoefu wa miaka mitano ya kucheza mechi za hatua ya makundi.

Iwapo vikosi vya Simba na Vipers, vingeundwa kwa kutegemea wachezaji wazalendo peke yao sioni namna ambayo Simba ingeweza kupata pointi zote sita.

Wigo mpana wa wachezaji wanaozalishwa katika ligi za ndani ni kazi ya uhakika inayofanywa na klabu.

FC Bamako, Monastir na TP Mazembe, klabu tatu vilizokuwa katika kundi la Yanga kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Vikosi vyao kwa mtazamo wa haraka, vinaundwa na wachezaji wengi walioandaliwa katika timu zao za vijana. Msingi wa timu hizo, unajengwa na wingi wa wachezaji wanaomilikiwa na klabu tangu wakiwa vijana wadogo.

Nimesikia kuwa mpango wa kukuza vijana utakaoanza kutekelezwa na Simba, utatumia sh. milioni 500 baada ya kuingia mkataba na Kampuni ya MobAd kudhamini timu za vijana kwa kaulimbiu ya 'The Future Is Now'.

> **Liliandaliwa kundi kubwa la wachezaji, lakini wengi wao wakiwa ni vijana wa hapa hapa Dar es Salaam. Waliweza kupatikana kwa urahisi, wakitokea nyumbani na kwenda kufanya mazoezi ya pamoja...**

Ni wa kuzunguka nchi nzima, kutafuta aina ya wachezaji watakaoingia moja kwa moja katika mtindo wa mpira wa Simba wa miaka yote. Hii sasa ni kazi halisi ya klabu ya soka.

TFF ikiwa ni Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini, haina jukumu la kukuza vipaji. Wao ni waratibu wa shughuli za kimpira za Tanzania. Wanafanya yale masuala ya usimamiaji wa mchezo.

Wao ni taasisi ambayo katika mataifa yaliyosimama imara kimpira hufanya shughuli za kiuongozi, zile za kuuweka hadharani mwelekeo mzima wa mchezo katika kipindi fulani.

Huwezi kusikia FA ya England imemuandaa mchezaji wa kiwango cha Bukayo Saka au Jude Bellingham. Barcelona walianza kumuandaa, Jerad Pique na sasa wamempika beki mwingine wa kati kijana.

Hawa wanaandaliwa katika viwanja vya mazoezi vya klabu vinazokua chini ya Chama cha Soka na wanakuwa moja kwa moja chini yao wakati wa mechi za kimataifa.

Leo hii kila mpenda mpira wa vionjo, analiimba jina la Clatous Chama na wengine wanafika mbali mpaka kumkabidhi mbuzi wanaokwenda naye uwanjani.

Ratiba ya mechi za kimataifa ilipotoka, Chama akapanda ndege na kwenda kujiunga na kikosi cha timu ya Taifa ya Zambia.

Angekua ni mchezaji Mtanzania, angekua mmoja wa sehemu ya timu yetu ya Taifa 'Taifa STars' ambayo leo hii kikosi hicho kinaikaribisha timu ya taifa Uganda katika mechi ya kutafuta tiketi ya kwenda kucheza michuano ya AFCON kule nchini Ivory Coast.

Ni sawa na namna kila shabiki wa Yanga, anavyojua kushangilia kwa mtindo wa mshambualiaji wao Fiston Mayele kila anapofunga goli.

Lakini Mayele, ameitwa katika kikosi cha DR Congo kwenda kutafuta nafasi ya kushiriki michuano ijayo ya AFCON.

Chama na Mayele, mpaka kufika hatua ya kupanda ndege kwenda nchi jirani kutafuta maisha ni kazi iliyofanywa katika viwanja vya mazoezi vya klabu vilizowakuza kimpira huko Zambia na DRC.

Wajibu wa kumkuza mchezaji mzuri, unaanzia katika klabu zetu. Hauwezi kuwa ni wajibu wa TFF.

Wao wakiwa ni Shirikisho la Soka, kazi yao ni kutaja majina ya wachezaji kwa ajili ya mechi za kalenda ya CAF na Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Miguu (FIFA) na wakishamaliza kucheza, wanawarudisha katika klabu zao husika.

Azam wamekua na juhudi za kukuza mpira, ambazo ni matumizi ya pesa nyingi za ligi ya vijana kila msimu. Yanga na Simba watafanya la maana sana, iwapo watawasaidia Azam katika kuandaa wachezaji halisi watakaokua sababu ya mashabiki kujivunia.

Wakati mwingine unajikuta ukishangaa tu namna shabiki wa Yanga au Simba anavyomkosoa mchezaji aliyelelewa na timu nyingine, wakati timu yake haijawahi kumuandaa wa aina hiyo.

Umefika wakati wa klabu hizi kutokwepa jukumu la moja kwa




# Kagi nyekundu aliyopewa Doucoure yaibua mjadala

**LONDON, England**

KADI nyekundu aliyolimwa mchezaji Abdoulaye Doucoure kwa kosa la kumshika machoni Harry Kane wa Tottenham Hotpusr imeibua mjadala. Doucoure alimvamia Kane baada ya kutokea mzozo baina yao, katika mechi waliyotoka sare ya bao 1-1, juzi usiku. Baadhi ya wachezaji wakieemo Piers Morgan na Jamie Carragher wameguswa na tukio hilo na wamemshukia Kane kwa kitendo chake cha kujiangusha ili kumuhadaa mwamuzi.

Kane baada ya kushikwa machoni, alianguka chini kumshawishi mwamuzi kumpa kadi nyekundu Doucoure.

Kwa tafsiri ya wachambuzi hao waliona kuwa Kane alilikuza tukio hilo. Doucoure alimfanyia madhambi Kane muda mfupi baada ya kuchezewa rafu na Demarai Gray.

Kane na Doucoure walivutana jezi kabla ya kocha wa Everton kuwaamua, hata hivyo nahodha huyo wa England ëalijiangushaí.

Wachambuzi hao wanakiri Doucoure alitenda kosa, lakini Kane hakutakiwa kufanya tukio hilo la kumshawishi mwamuzi aonekane ameumia zaidi.

Kiungo wa zamani wa Spurs, Danny Murphy alisema Kane ni kama alilikumbatiaí tukio hilo kwa kuwa hakustahili kuanguka.

Harry Kane hakupaswa kuanguka, si tukio la kumfanya aende chini ingawa Doucoure alifanya kosa na alistahili kadi nyekundu.

# Pochettino miongoni mwa majina yanayotajwa kumrithi Potter Chelsea

**LONDON, England**

JINA la Mauricio Pochettino ni miongoni mwa majina makubwa yanayotajwa kurithi mikoba ya Graham Potter kuinoa Chelsea.

Pia wamo Luis Enrique, Julian Nagelsmann na Roberto De Zerbi ambao wameingia katika orodha ya kuwania kibarua Stamford Bridge.



Chelsea ina idadi kubwa ya orodha ya makocha wanaotajwa kumrithi Potter, lakini haijafikia mwafaka nani kubeba dhamana hiyo ingawa Nagelsmann anapewa nafasi.

Enrique na Pochettino wana rekodi nzuri katika soka hatua inayoweza kutoa wakati mgumu kwa vigogo wa klabu hiyo kuchagua jina moja kati ya makocha hao.

Urafiki wa Nagelsmann na mmiliki wa klabu hiyo unampa nafasi ya kuvaa viatu vya Potter ingawa umri wake wa miaka 35 umeleta mjadala.

Enrique hana kazi tangu alipotimuliwa kuinoa Hispania muda mfupi baada ya kuaga kwa aibu fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar.

Kwa upande wake Pochettino tangu alipoinoa Paris Saint-Germain msimu uliopita wa majira ya kiangazi hana timu.

Pia Pochettino anatajwa kurejea Tottenham Hotspurs huku Real Madrid ikiwemu katika rada zake kwenda kujaza nafasi ya Carlo Ancelotti.

Rais wa Real Madrid Florentino Perez inataka kufanya mabadiliko msimu ujao kwa kumuajiri kocha mwenye uzoefu.




# Mechi ya Everton, Tottenham ya kwanza kutoa nafasi wachezaji kufuturu

**LONDON, England**

MECHI ya Everton dhidi ya Tottenham Hotspurs imekuwa ya kwanza katika Ligi Kuu England msimu huu kusimama kwa muda kutoa nafasi kwa wachezaji wa dini ya kiislamu kufuturu.

Miongoni mwa wachezaji waliopata fursa hiyo katika mwezi huu wa mfungo wa Ramadhani ni Andre Onana, Abdoulaye Doucoure na Idrissa Gueye.

Mechi za Ligi Kuu England zitakuwa zikisimama kwa muda mfupi kuruhusu wachezaji waislamu kula na kunywa kabla ya kuendelea na mchezo.

Katika hatua nyingine, kocha Thomas Tuchel ana matumaini Sadio Mane atacheza kwa kiwango bora Bayern Munich ingawa ameanza msimu kwa kusuasua.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Liverpool na nyota wa Senegal, ndiye tumaini la klabu hiyo ya Allianz Arena, lakini bado hajaonyesha makali.

Mane amefunga mabao 11 katika mchi 29 za mashindano yote aliyocheza,

# ZAA yafurahia wachezaji wake kuitwa Timu ya Taifa

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

CHAMA Cha Riadha Zanzibar (ZAA) kimeelezea furaha yake baada ya wachezaji wake saba kuitwa katika timu ya Taifa ya Tanzania, itakayoshiriki michuano ya Afrika inayotarajiwa kufanyika nchini Zambia mwezi huu.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi Katibu Msaidizi wa chama hicho, Muhidini Yasin alisema wachezaji hao walipatikana baada ya kufanya vizuri na kufikia vigezo vilivyohitajika kuwa mchezaji wa timu ya taifa katika mashindano ya wazi yaliyofanyika mwishoni mwa mwezi uliopita.

Alisema ni jambo la kujivunia na kuwapongeza viongozi wa taassisi ambazo wachezaji wake wametoka kuunda timu hiyo.

Ni jambo la faraja kwetu sisi na huu ni wazi kwamba kuna ushirikiano wa kutosha kwa viongozi wa taasisi hizo, ambazo kwa namna moja wamekuwa wakifanikisha mipango ya wachezaji hao.

Wachezaji hao watatu wametoka katika timu za Mafunzo wawili KMKM, JKU na Polisi wakitoa mchezaji mmoja mmoja .

Kiukweli niseme tu kwamba taassi hizo zinahitaji kushukuriwa kwani zimekuwa zikiwapa muda wa kutosha wachezaji wao kushiriki mazoezi,î alisema Yasin.

Hata hivyo alisema mbali ya ushirikiano huo, lakini pia wamefanikiwa kutokana na juhudi kubwa ambazo wamekua wakizifanya ikiwemo kushiriki mazoezi.

Wachezaji walioitwa ni Hamad Ali, Nasra Abdalla na Ali Hamad wote kutoka timu ya Mafunzo, Gasisi Geagasa (Polisi), Hafidh Talib na Mwanamie Khamis Hassan (KMKM) na Samir Mbaraka Sururu (JKU).

## Kamati ya Utendaji ZAA kukutana leo

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

UONGOZI wa Kamati ya Utendaji ya Chama cha Mpira wa Wavu Zanzibar (ZAVA), unatarajiwa kukutana leo kujadili usajili na kupitia kanuni ya kuendesha ligi.

Hayo yalisemwa na Katibu Msaidizi wa chama hicho, Eutist Mwakanjuki alipozungumza na mwandishi wa habari hizi kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu chama hicho.

Alisema kikao hicho kitafanyika mafunzo Kilimani Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na kushirikisha viongozi wote wa Kamati ya Utendaji. Pia katika kikao hicho watapitia kanuni hiyo kwa kuangalia vipengele vya kanuni hiyo na kuvifanyia marekebisho kwa vile ambavyo vitahitaji kufanyiwa hivyo.

Hata hivyo alisema, wanafanya hivyo ikiwa ni kuanza maandalizi ya Ligi ya Kanda ya Unguja itakayoanza Julai pamoja na Ligi kuu ya Zanzibar ambayo itaanza Oktoba mwaka huu.



Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud akizungumza na viongozi wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Mkoa huo waliofika ofisini kwake kuzungumzia maendeleo ya soka. Na Mpigapicha Wetu

## Uvuvi wakwamisha vija kupenda michezo Kizimkazi

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

KIJIJI cha Kizimkazi Dimbani licha ya kuwa na vijana wengi wenye vipaji, lakini vinaja hao wamegoma kushiriki michezo hasa mpira wa miguu na vijana wengi kujikitia katika uvuvi na utalii.

Hayo yalisemwa na mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Badru Simai Haji alipozungumza na mwandishi wa habari hizi kuhusiana na hali ya michezo ndani ya kijiji hicho baada ya timu ya Dimbani Stars kufa.

Vizazi vingi vya Kizimkazi lazima niseme ukweli kwamba bahari, utalii vimechangia na hawaweki mpira mbele kutokana na hali tuliyo nayo katika kijiji chetu,î alisema.

Alisema kuna vijana wengi, lakini na wao wameacha moja kwa moja kushiriki ligi na badala yake michezo ambayo wanashiriki ni yale yanayoandaliwa ndani ya kijiji hicho pekee.

# Polisi Jamii Cupa yashika kasi Pwani

**Na Mwandishi Wetu, Chalinze**

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani kupitia Kamanda wake, Pius Lutumo limeandaa ligi ndogo ijulikanayo kwa jina la Polisi Jamii Cup, inayolenga kuimarishwa kwa ulinzi mkoani hapa.

Ligi hiyo ndogo ya mpira wa miguu ni maandalizi ya mashindano yanayotarajiwa kuanzishwa na jeshi hilo, itakayochezwa katika wilaya zote saba na majimbo mawili yanayounda Mkoa wa Pwani.

Ligi hiyo ndogo imechachezwa katika wilaya kadhaa, huku mwishoni mwa wiki imepigwa fainali kati ya Chalinze Mzee dhidi ya Chalinze Academy, ambapo Chalinze Mzee, imetwaa mbuzi wawili baada ya kuwafunga Chalinze Academy kwa penalti 4-2.

Penalti hizo zilipigwa baada ya kutoka sare ya bao 1-1, ambapo bingwa alijinyakulia mbuzi wawili, msindi wa pili mbuzi mmoja, ambapo baada ya fainali hiyo Afisa Mnadhimu Ushirikishwaji wa Polisi na Jamii Kamishina Msaidizi ACP Michael Manumbu alisema lengo la mashindano kuiimarisha ulinzi.

“Kamanda wa Polisi mkoani kwetu Pius Lutumo ameanzisha ligi hii ndogo ikiwa ni maandalizi ya ligi kubwa itayochezwa mkoa mzima kwa kuanzia ngazi za Wilaya lengo kuwa karibu na wananchi, hatua itayosaidia kuwawezesha wananchi kuwataja waharifu,” alisema Manumbu.

Katika kituo cha Chalinze timu zilizoshiriki ni nne, ambazo mbali ya Chalinze Mzee ambao ndio Bingwa na mshindi wa pili Chalinze Academy, nyingine zilizoshiriki ni Dawasa Fc na Pera Star ambazo zilishindwa kutinga fainali hiyo.



# Kuionea TFF ni kutegemea kuzalisha Stars ya baadae

Uk. 20

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumanne Aprili 5 - 11, 2013 |



# Mechi ya Everton, Tottenham ya kwanza kutoa nafasi wachezaji kufuturu

Uk. 22



# Simba, Yanga zapanda viwango vya CAF

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU za Simba na Yanga, zimepanda katika viwango vya ubora kwenye michuano ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), baada ya kukamilika kwa hatua ya makundi ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho

Klabu ya Simba yenyewe imepanda kwa nafasi nne, kutoka nafasi ya 11 mpaka nafasi ya 7.

Simba ni miongoni mwa timu nane zilizofuzu robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa, wakisubiri droo ya mechi za robo fainali itakayopigwa leo nchini Misri.

Yanga kwa nafasi ya 26 kutoka nafasi ya 46 mpaka nafasi ya 20, baada ya kufanikiwa kutinga robo fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho.

Kwa mara ya kwanza Yanga, imeingia katika klabu 20 bora barani Afrika. Klabu hiyo inaweza kusogea juu zaidi kama watafanikiwa kuvuka hatua ya robo fainali.



## Yanga yawashukuru mashabiki waliojitokeza Lubumbashi

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Klabu ya Yanga umewashukuru mashabiki na wanachama waliojitokeza Uwanja wa TP Mazembe mjini Lubumbashi nchini DR Congo, katika mchezo wa mwisho wa Kundi D Kombe la Shirikisho Afrika uliopigwa Jumapili.

Yanga iliyokua ugenini, ilifanikiwa kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya wenyeji wao TP Mazembe, bao la ushindi likifungwa na kiungo mshambuliaji, Farid Mussa katika kipindi cha pili.

Kupitia kurasa za mitandao ya kijamii za klabu hiyo, uongozi umewasilisha neno hilo la shukurani kwa mashabiki na wanachama wa klabu hiyo, ambao wengine walilazimika kusafiri kutoka jijini Dar es Salaam kwa usafiri maalum wa basi.

Shukrani na pongezi kwa wanachama, mashabiki na wapenzi wa Yanga, Congo mmekuwa watu wema na msaada mkubwa kwetu.



Wote waliosafiri kuja kutupa nguvu na sapoti, mtaishi milele kwenye historia ya klabu yetu na kuwa sehemu ya mafanikio yetu, pamoja na wote waliokua wanatuombea na kutusapoti wakiwa nyumbani.

Hakika jeshi la wananchi lilihamia Congo,î ilieleza sehemu ya taarifa iliyochapishwa mtandao huo wa Yanga.

Ushindi wa bao 1-0 dhidi ya TP Mazembe, umeifanya Yanga kumaliza kinara wa Kundi D, ikifikisha alama 13 sawa na US Monastir iliyoifunga AS Real Bamako 2-1 Jumapili nchini Tunisia.

Kwa mantiki hiyo Yanga, itakutana na moja ya timu zilizomaliza nafasi ya pili katika Kundi A, B na C Kombe la Shirikisho Afrika.

Timu hizo ni Rivers United ya Nigeria, Pyramids ya Misri au USM Alger ya Algeria.